

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 9 Juni, 2005**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

**DUA**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:**

Taarifa ya Kumi na Tisa na Hesabu za Bodi ya Tumbaku Tanzania kwa Mwaka ulioishia tarehe 31 Machi, 2004 (*The 19<sup>th</sup> Annual Report and Accounts of the Tanzania Tobacco Board for the Year ended 31<sup>st</sup> March, 2004*).

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 21

**Utaratibu wa Kutengeneza Barabara**

**MHE. JACOB SHIBILITI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa na utaratibu wa kutengeneza barabara zake wakati wa ujio wa viongozi wa kitaifa, kama ilivyotarajiwa wakati wa ujio wa Mtoto wa Mfalme wa Norway, na kwa kuwa, kwa taarifa hizo Serikali iliamua kupeleka greda kutengeneza barabara ya Kabale hadi Ng'obo ambayo ilianzwa kutengenezwa lakini haikukamilishwa kutokana na kuahirishwa kwa ujio huo kwenye maeneo hayo na matokeo yake barabara hiyo iliachwa ikiwa na hali mbaya, madaraja kuahirishwa na sasa haipitiki kabisa:-

(a) Je, Serikali inafahamu uharifu huo;

- (b) Je, ni nani anawajibika kutengeneza barabara hiyo kati ya Halmashauri na Serikali Kuu.
- (c) Baadhi ya vibarua hawakulipwa fedha zao, Je, ni nani anawajibika kuwalipa vibarua hao na watalipwa lini.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI  
ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Shibili, Mbunge wa Misungwi lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Serikali inatambua vyema uharifu ulioko kwenye barabara ya Kabale – Ng'obo pamoja na barabara nyingine zilizoko Wilayani, lakini kutokana na uhaba wa fedha na nyenzo muhimu za kuzifanyia matengenezo barabara zote kwa wakati mmoja, hii ndio sababu inayopelekea barabara hiyo kufikia kiwango hicho cha uchakavu.
- (b) Mheshimiwa Spika, barabara ya Kabale – Ng'obo ni barabara ya Wilaya, hivyo Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi inawajibika kuifanyia matengenezo, ili iweze kupitika muda wote. Barabara hii iko katika hali mbaya kiasi kwamba inahitaji kukarabatiwa au *rehabilitation*. Hata hivyo kwa mujibu wa Sheria ya ushuru wa barabara Na. 13 ya mwaka 1985 *The Road Tolls that No. 30 of 1985* kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Marekebisho ya ushuru wa barabara Na. 2 ya mwaka 1998 kifungu cha (4) kifungu kidogo cha (3) cha Sheria hiyo, kinasisitiza kuwa fedha zamfuko wa barabara zinatakiwa kutumika katika kazi za matengenezo ya maeneo muhimu matatu, kwanza ni maeneo korofi kwa maana ya *Spot Improvement*, Matengenezo ya kawaida yaani *Routine Maintenance* na Matengenezo ya Muda yaani *Periodic Maintenance* na siyo ukarabati.

Aidha, katika kifungu hicho cha (4) kifungu kidogo cha (5) cha sheria hiyo kinakataza matumizi ya fedha za Mfuko huo katika maeneo zaidi ya yale yaliyoainishwa kwenye Sheria. Kwa kuwa fedha zinazotolewa na Mfuko wa Barabara huwa ni za aina ya matengenezo ya barabara zilizoainishwa kwenye Sheria, Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi huifanyia barabara hiyo matengenezo ya sehemu kama nilivyoleza hapo juu na sio vinginevyo na kulingana na uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Halmashauri ya Wilaya Misungwi sasa imekamilisha matengenezo ya eneo korofi kwenye tuta la Ng'obo mita 400 lililokuwa ni kikwazo kubwa katika barabara hiyo kwa gharama ya shilingi milioni 9 na hivyo kuiwezesha barabara hiyo sasa kupitika.

(c) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi haijapokea malalamiko toka kwa mtu ye yeyote kuhusu kutokulipwa fedha zinazohusiana na matengenezo ya barabara hiyo. Ikiwa kuna mtu/watu wenyewe madai ya namna hiyo wayawasilishe madai yao kwenye Halmashauri, yakidhihirika kuwa ni halali yatalipwa.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza kabisa nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri na pia nimpongeze yeye na Serikali kwa ujumla kwa kazi nzuri iliyofanyika kwa barabara ya Ilalabogo Isenengeja, Ibiza na Mwawile nawapongeza sana kwa kazi nzuri hiyo iliyofanyika.

Swali la kwanza kwa kuwa Waziri amekiri kwamba kweli barabara ya Kabale Ng'obo ni tatizo kubwa na wametengeneza mita 400 kati ya kilometra 9 ambazo zilikuwa zimekisiwa kutengenezwa.. Je, sehemu iliyobaki itatengenezwa lini?

La pili kwa kuwa nina ushahidi kabisa wa watu ambao bado wanadai pesa zao zaidi ya laki sita, Waziri unanisaidiaje ili wananchi hao waweze kulipwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nipokee kwa mikono miwili pongezi alizozitoa kwa kazi nzuri iliyofanywa. Lakini nadhani zingestahili kupelekwa zaidi kwenye Halmashauri yake kwa sababu ndio wamefanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba barabara ndio niliyotaja inapitika vizuri. Kuhusu maswali yake mawili;

Kwanza hili la matengenezo ya barabara sasa kwa maeneo yaliyobaki, ninaomba tu Mheshimiwa tushirikiane kinachohitajika hapa ni kuweka kipau mbele katika maeneo ambayo unaona barabara inastahili yaingizwe kwenye mpango wenu wa Halmashauri ya Wilaya Misungwi kisha iwasilishwe katika ofisi yetu na madamu tumelivalia njuga basi na sisi tutahikikisha tunalizingatia wakati wa kupanga mipango yetu.

Lakini la pili kuhusu hawa watu wanaodai kiasi cha shilingi laki sita, Mheshimiwa Mbunge madamu unayo orodha na ushahidi mimi sioni kama kuna tatizo hata kidogo ninakuomba ama uwasilishe orodha hiyo kwenye Halmashauri yako na ushirikiano nayo kuhakikisha kwamba fedha hizo zinalipwa na ukiona ni vyepesi kutumia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ruksa fanya hivyo na tutakusaidia.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu huu awa *adopt* kuupeleka fedha za barabara kwenye Halmashauri ni utaratibu mzuri sana na umesifiwa na baadhi ya Wabunge, lakini nina swali moja dogo la nyongeza.

Je, Waziri kwa sababu ya kusimamia vizuri Waheshimiwa Wabunge unawenza ukaanzisha utaratibu kama ule *TANROAD* wa Wizara ya Ujenzi kutupa taarifa ya fedha

inayokuja Wilayani ili zisije zikashindikana kufuatilia kwa kuwa Halmashauri vikao vyake ni vichache mno tuweze kufuatilia.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali ilishatoa maagizo kwenye Halmashauri zote kuhakikisha kwamba fedha hizi zinazopelekwa katika Halmashauri zao lazima ziwekwe kwenye matangazo ya kawaida katika maeneo ya ofisi zao, ili kuwezesha kwanza wananchi wa kawaida tu kuweza kujua kiasi cha fedha ambazo zimepelekwa katika Halmashauri zao. Sasa inawezekana jambo hili halijatekelezwa kikamilifu lakini tutaendelea kulisukuma ili lifanyike.

Lakini pili kuhusu rai aliyoitao nafikiri halina tatizo tutaliwasilisha katika ofisi yetu watendaji waweze kuzingatia hilo kwa wakati uanokuja.

Na. 22

### **Barabara Jimbo la Mlalo**

**MHE. CHARLES H. KAGONJI** aliuliza:-

Kwa kuwa mafuriko na maporomoko ya mwaka 1993 yaliyotokea Wilayani Lushoto na baadaye mvua za muda mrefu za *El-Nino* zilivunja na kuathiri kwa kiwango kikubwa miundombini mbalimbali ikiwemo ya Barabara katika Jimbo la Mlalo na kwa sababu Barabara za changarawe sasa zimegeuka kuwa za vumbi na kuleta usumbufu mkubwa wakati wa mvua kiasi cha magari mengi ya mizigo na abiria kukwama njiani na hivyo kusababisha mateso makubwa kwa wananchi:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kurejesha changarawe kwa Barabara za Mkoa za Jimbo la Mlalo zilizopatwa na mikasa hiyo;
- (b) Je, tangu kipindi hicho Barabara za Magamba – Malindi – Mlalo, Malindi – Rangwi – Nkelei na Lukozi – Mamolo – Mtae zilifanyiwa matengenezo ya namna gani;
- (c) Je, Serikali inafahamu kuwa Barabara hizo hupitisha uzito mkubwa sana kwa siku kama vile mabasi ya abiria makubwa na madogo, malori ya mizigo mbalimbali kama magogo, mbao, matunda, viazi mviringo, mboga na pia maharage.

### **NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Charles Kagonji, Mbunge wa Jimbo la Mlalo, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Mlalo lililopo Wilaya ya Lushoto, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) inahudumia Barabara za Lushoto – Mlalo yenyewe urefu wa kilometra 40, Lukozi – Nkelei yenyewe urefu wa kilometra 22.5 na

Malindi – Mtae yenye urefu wa kilometra 30. Ni kweli Barabara hizi pamoja na Barabara nyingine za Wilaya hiyo zilipata athari mbalimbali wakati wa mafuriko makubwa ya mwaka 1993 na mwaka 1998.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutumia fedha zake za ndani na za wahisani mbalimbali hususani, Serikali ya Norway na Denmark kupitia Mashirika yake ya misaada ya NORAD na DANIDA, iligharimia matengenezo ya dharura katika Barabara hizo hadi zikapitika. Aidha, Serikali inaendelea kuzifanyia matengenezo Barabara hizo kwa kuziwekea changarawe baadhi ya sehemu korofi kama ifuatavyo:-

Katika mwaka wa fedha 2001/2002 na 2002/2003 barabara za Lushoto – Mlalo kilometra 40, Lukosi – Nkelei kilometra 22.5 na Malindi – Mtae (kilometra 30 zilifanyiwa matengenezo ya Kawaida, matengenezo dharura na matengenezo ya sehemu Korofi kwa gharama ya shilingi milioni 183.8. Halikadhalika, katika mwaka 2003/2004 zilitumika jumla ya shilingi milioni 66.483 kwa matengenezo hayo. Mwaka wa fedha 2004/2005, Serikali imetenga shilingi milioni 71.885 na zimetumika shilingi milioni 51.01 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida na sehemu korofi ya barabara hizo.

Aidha, Serikali ilitenga jumla ya shilingi milioni 372 katika mwaka wa fedha 2003/2004 kwa ajili ya usanifu wa Barabara kwa kiwango cha lami pamoja na usimamizi wa kazi sehemu ya Lushoto – Magamba, katika barabara ya Lushoto – Mlalo. Kazi ya usanifu imekamilika na jumla ya shilingi 59.4 milioni zimetumika. Salio la shilingi 312.6 milioni la mwaka 2003/04 na shilingi 200 milioni zilizotengwa mwaka 2004/2005 zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa Barabara hiyo kwa kiwango cha lami na usimamizi. Mradi huu utaendelea kutengewa fedha katika miaka ijayo ya fedha hadi itakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, tayari Mkandarasi wa kujenga lami katika Barabara ya Lushoto – Mlalo sehemu ya Lushoto – Magamba tayari ameshapatikana na kazi ya ujenzi wa kilometra 1.5 ambayo ni awamu ya kwanza ilianza mwezi wa Aprili 2005 na itagharimu jumla ya shilingi 410.997 milioni na kazi itakamilika mwezi Oktoba, 2005.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa niyajibu maswali yake (a), (b) na (c) kwa kifupi sana.

- (a) Kutokana na ufinyu wa bajeti si rahisi kwa Serikali kuziwekea changarawe Barabara zote za Jimbo la Mlalo kwa mara moja. Kama nilivyoeleza katika maelezo ya jumla, Wizara itaendelea kuandaa na kutekeleza mipango ya muda mrefu na muda mfupi wa ujenzi na matengenezo ya Barabara mbalimbali ikiwa ni pamoja na Barabara za Jimbo la Mlalo kama ifuatavyo sasa.
- (b) Matengenezo yaliyofanyika katika Barabara za Jimbo la Mlalo zenyе jumla ya kilometra 92.25 tangu kutokea mafuriko ya mwaka 1993 na mvua za *El-Nino* mwaka 1998 ni ya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na matengenezo ya sehemu korofi ‘spot improvement works’, matengenezo ya dharura na matengenezo ya

kawaida *routine maintenance works* kama nilivyoeleza katika maelezo ya utangulizi.

- (c) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kuwa, Barabara ya Lushoto – Mlalo inapitisha jumla ya wastani wa magari 195 kwa siku, Barabara ya Lukozi – Nkelei wastani wa magari 60 kwa siku na Barabara ya Malindi – Mtae wastani wa magari 80 kwa siku. Magari ya mizigo yanayopita katika Barabara hizi, mengi yakiwa aina ya Fuso yanabeba mzigoto usiozidi tani 15. Aidha, Serikali inafahamu kuwa maeneo ya Lukozi, Manolo, Nkelei na Mlalo ni maarufu katika Wilaya ya Lushoto kwa uzalishaji wa mazao mbalimbali kama vile viazi mviringo, mboga za kila aina na matunda.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulieze maswali madogo mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningemba nimuulize kama ifuatavyo;

Barabara hizi nilizozieleza hapa zimepata madhara, na kwa kweli ni kama mtu aliyepata ajali, yale mafuriko na maporomoko ni ajali kubwa ambayo yalichukua sehemu kubwa ya changarawe, halafu na mvua hizo za *El-Nino*. Je, Waziri anasema Serikali haiwezi kutengeneza barabara zote kwa mara moja lakini kwa sababu barabara hizi zilikuwa za changarawe toka mwanzo. Sasa Serikali inajiaandaa kutengeneza sehemu gani au barabara kiasi gani kwa mwaka huu wa fedha ili kuondoa taratibu hilo tatizo ambalo linawasibu wananchi wa jimbo la Mlalo. La pili naomba kuuliza kwamba barabara ya Mkomazi, Mnazi Humba ina tatizo kubwa la lile daraja letu la Mkundi. Mara kwa mara Serikali imenipa matumaini na Wizara hii kwa kweli tumeshirikiana lakini bado naona hali ya daraja wala halijaanza kujengwa. Je, Serikali inasemaje kuhusiana na daraja lile la Mkundi na barabara ile ya sehemu za bondeni ya Mkomazi, Mnazi, Humba. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu nilieleza kwamba Serikali inajitahidi kutengeneza barabara hizi kwa kiwango cha changarawe kwa kadri fedha inapopatikana na tumekwisha rudisha sehemu kubwa sana changarawe hizo katika barabara hizo, na uwezo wa Serikali ni fedha na tunagawana sungura kwa nchi nzima. Kwa kweli kabisa *El-Nino* ziliwapiga 1998/1993 lakini hata hivyo Mheshimiwa Kagonji atakubaliana na sisi kwamba tumejitahidi kwa kiwango kikubwa sana kutengeneza, mpaka tumekwenda katika hatua ya kuwaomba *NORAD* na wengine ili watusaidie katika kutengeneza barabara hizo. Kwa hiyo, wananchi wa Mlalo naomba vile vile waelewe kwamba tunajitahidi sana kurudisha changarawe katika barabara hizo. Barabara ya Mkomazi, Mnazi hadi Humba na daraja la Mkundi.

Mheshimiwa Spika, daraja hili tumezungumza sana na Mheshimiwa Kagonji na barabara hii, lakini vile vile naomba wananchi wa Mlalo wakubali kwamba Mbunge wao anafuutilia sana daraja la Mkundi, na Wizara inajitahidi kwelikweli kupanga pesa kutengeza daraja hili. (*Makofii*)

### **Ujenzi wa Barabara ya Kyamyorwa - Buzirayombo – Geita**

**MHE. ERNEST GAKEYA MABINA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeingia mkataba wa ujenzi wa barabara ya kutoka Kyamyorwa – Buzirayombo hadi Geita kwa kiwango cha lami; na kwa kuwa ujenzi huo unakusudiwa kuanzia Usagara hadi Kyamyorwa ili kuhimili magari makubwa yanayopeleka mafuta kwenye mgodi wa Geita:

Je, Serikali imetumia kigezo gani cha kubadili uamuzi wa awali na kuanza ujenzi huo kuanzia Kyamyorwa badala ya Usagara?

- (a) Je, kile kipande kilichobaki cha kutoka Geita hadi Usagara kitajengwa lini?
- (b) Je, barabara hiyo itapindishwa na kupita nje ya miji kama ilivyofanyika katika miji ya Misungwi na Magu?

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mbunge wa Geita, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara hii ni utekelezaji wa Mpango Maalum uliobuniwa na Serikali kuititia Wizara yangu wa kujenga barabara kwa kiwango cha lami kwa kutumia fedha za mapato ya ndani. Lengo kubwa hapa ni kujijengea uwezo wa Kitaifa wa kugharamia miradi yetu wenyewe na kujaribu kuondokana na yale mazoea ya awali ya kuwa tegemezi kwa wahisani wa nje. Kwa yale maeneo ambayo utekelezaji wa mpango huu umeshaanza, matokeo yake yamekuwa ni ya kuridhisha sana kwani ule urasimu unaoambatana na matumizi ya fedha za Wahisani haupo tena. Pia, miradi hii inatekelezwa kwa utaratibu wa *Design and Build* ambao huokoa muda na gharama.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya Kyamyorwa – Buzirayombo hadi Geita umepangwa kufanyika katika awamu mbili. Awamu ya kwanza inazo barabara zifuatazo:
  - ◆ Kyamiorwa - Buzirayombo (kilometra 120).
  - ◆ Buzirayombo – Geita. (Kilometra 100).

Kwa wakati huu, Makandarasi tayari wapo katika maeneo yao ya kazi wakifanya usanifu na kijiandaa kuanza kazi rasmi. Awamu ya pili inazo barabara zifuatazo:

- ◆ Geita – Usagara (kilometra 92).
- ◆ Bwanga - Biharamulo (kilometra 60).

Hatua ya utekelezaji iliyofikiwa ya awamu hiyo pili ni ile ya kumtafuta Mhandisi Mshauri (*Consultant*) wa kuzifanya usanifu wa kina ili kubaini gharama halisi za utekelezaji wake. Mkataba husika utasainiwa mwezi Juni, 2005.

Hivyo basi azma ya Serikali ya kujenga barabara hii yote kwa kiwango cha lami ni thabiti bila kujali mahali barabara inapoanza. Utekelezaji wake tayari umeshaanza kwa awamu, na huo ndio uliokuwa mpango wa Serikali na *design* inayofanywa sasa na Mkandarasi imeanzia Geita kuelekea Buzirayombo na Kyamiorwa.

- (b) Kama nilivyoeleza katika sehemu (a) hapo juu, barabara ya Geita – Usagara (kilometra 92) imepangwa kutekelezwa katika awamu ya pili ya mradi huu. Mara tu Mhandisi Mshauri atakapokamilisha kazi yake, Serikali itatangaza zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.
- (c) Mkataba uliosainiwa kati ya Serikali na Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya Buzirayombo hadi Geita utahusisha kujenga barabara mpya ya lami itakayopita nje ya mji wa Geita kama ilivyofanyika katika miji ya Misungwi na Magu.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa niulize swali la nyongeza. Kwanza napenda kuipongeza Serikali kwa kutuma mapato yake ya Taifa kuweza kutujengea barabara ya lami kutoka Kyamiorwa mpaka Geita.

Pili kwa sababu sasa hivi kuna wingi wa magari ambayo yanatoka Mwanza kuja mpaka Geita ambayo yanabeba mafuta na barabara ya kutoka Usagara mpaka Geita inakuwa inatengenezwa mara kwa mara. Je, Serikali inasemaje badala ya kusubiri subiri mpaka awamu ya pili ikajenga barabara hiyo haraka iwezekanavyo ili kuepukana na uharibifu wa mara kwa mara wa magari?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kupokea shukrani kwako Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya Wizara kwa niaba ya Waziri wangu naipokea. Swali linahusu utengenezaji wa barabara hii haraka iwezekanavyo ili tuweze kumaliza, kwa hakika Wizara ya Ujenzi ingependa kujenga barabara hizi haraka sana.

Lakini moja, kinachotawala ujenzi wa barabara taratibu zifuate, ama sio tutatengeneza barabara mbovu kupita kiasi.

La pili, ni upatikanaji wa fedha ambazo lazima ziende katika mtiririko, hizi ni fedha zetu za hapa nchini tunazipanga polepole na moja ya mpango wa kupata fedha hizi uko katika bajeti hii inayokuja. Kwa hiyo, tutakuomba Mheshimiwa Mbunge utusaidie kuipitisha bajeti hii ili tuharakishe kwenda.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swalii moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa sambamba na ujenzi wa barabara hii ya Usagara hadi Geita na Kiambro kwa kiwango cha lami, Wizara ya Ujenzi ina mpango wa kununua kivuko kipyaa cha Kigongo na Busisi na kwa kuwa kivuko kilicho sasa hivi kimechoka kinazimika katikati ya maji na kinatia uwoga kupanda. Je, Serikali itatuambia ni lini kivuko kitakuwa tayari na kitakuwa na ukubwa gani tofauti na kile kilichopo sasa hivi?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba swalii la msingi la Mheshimiwa Mabina lilikuwa linazungumzia barabara ya Usagara kwenda Kyamiorwa, na alikuzungumzia feri, lakini napenda nitoe taarifa kwa Mheshimiwa Musalika kwamba kivuko cha Kigongo hadi Busisi *tender* zimeshatangazwa na kandarasi amekwisha patikana, kampuni moja ya Senetio kutoka Uholazi. Kivuko hicho kitanunuliwa kwa gharama ya bilioni 3.7, na kivuko hicho kitakuwa na uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 1000, magari makubwa ya *semitera* zaidi ya sita na magari madogo madogo 26. (*Makofî*)

Hicho kivukoa kinategemewa kuingia katika kipindi cha miezi kumi hadi kumi na nne kuanzia siku mkataba uliposainiwa. Kwa hiyo, napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ujenzi wa barabara ya Usagara hadi Kyamiorwa inaendana pia na ununuzi wa kivuko ambaa utasaidia katika usafirishaji. Lakini pia kilichopo sasa hivi ni salama na kinatumika kulingana na ratiba iliyopo. (*Makofî*)

Na. 24

### **Matengenezo ya Barabara Nchini**

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kutokana na juhudii zinazoendelea sasa za ujenzi wa barabara za lami; Serikali imelazimika kujenga upya baadhi ya barabara za lami ambazo zilitengenezwa miaka ya nyuma kama vile barabara ya Chalinze- Morogoro –Mikumi na Songwe – Tunduma:-

- (a) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba matengenezo hayo yametokana na kukosekana kwa matunzo ya mara kwa mara ya barabara husika;
- (b) Je, baada ya matengenezo hayo, na pia baada ya kukamilika kwa barabara mpya za lami, kutaku wana mipango gani ya matunzo ya barabara hizo.

## **NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, ukarabati unaoendelea kwenye barabara zilizojengwa huko nyuma unatokana na kwisha kwa umri wa matumizi '*life span*' wa barabara husika. Kwa mfano, barabara ya Dar es Salaam - Chalinze -Morogoro – Mbeya – Tunduma wakati wa ujenzi ilikadiriwa kutumika kwa muda wa miaka 15 tu baada ya kukamilika ujenzi miaka ya 1972/1973. Lakini barabara hii imetumika zaidi ya miaka 30, umri huu umefikiwa kutokana na matengenezo ya mara kwa mara kwenye barabara husika ingawaje matengenezo hayakufanyika katika muda unaotakiwa ambayo yanepunguza gharama za kuongeza umri wa matumizi kulinganisha na gharama za kuongeza umri wa matumizi kulinganisha na gharama zinazotumika kukarabati kwa sasa. Hii yote imetokana na uwezo mdogo wa uchumi wa nchi yetu.
- (b) Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kuhakikisha kuwa mara barabara inapokamilika kujengwa au kukarabatiwa, itaendelea kufanyiwa matengenezo ya mara kwa mara yaani *Routine Maintenance* na maalum *Periodic Maintenance* ili barabara ziendelee kudumu na kufikia umri zaidi ya miaka iliyotarajiwa. Fedha za Mfuko wa Barabara ulioanzishwa maalum kwa kazi hiyo zitatumika na ndio zinazotusaidia.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Kwa kuwa kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri amekubali kwamba ni kweli matengenezo haya makubwa yametokana na kutokufanya matengenzo wakati ule ule au wakati muafaka. Lakini vile vili Waziri atakubaliana nami kwamba baadhi ya wakandarasi wanaopewa ujenzi wa barabara wanapotengeneza barabara hizi zinakuwa mara nyingine si imara sana na kusababisha matengenezo kuanza mapema au kabla ya wakati uliopangwa, anakubaliana kwamba hilo ni tatizo pia?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara nyingi zinapotolewa *tender* tayari zimekwisha fanyiwa *design* na tayari imeshajulikana na kiwango gani cha ugumu na ubora wa barabara itakayofanyika. Kwa hiyo, mkandarasi anapotengeneza barabara ambayo ni duni mara nyingine si kosa lake, ni kosa la msimamizi *consultant* ambaye hatusaidii sana Serikali kwa maana hiyo. Lakini kwa kawaide mkandarasi atafuata maelekezo ya *design* na *consultant* anatakiwa asimamie kusaidia Serikali, kuhakisha kwamba pesa zinazotegemewa kutengeneza barabara hiyo zinatengeneza barabara ilivyotakiwa.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa barabara iliyotajwa inapita Mkao wa Iringa na kwa kuwa si muda mrefu barabara ya Milima ya Kitonga ilitengenezwa vizuri, sasa limejitokeza tatizo wakati mvua zinaponyesha barabara hiyo huteleza na kusababisha accident nyingi. Je, Wizara yako itakuwa tayari kwenda kuangalia tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, tumepata taarifa ya tatizo hilo Wizarani na tumetuma Mtaalam wetu *Regional Manager* wa Iringa akaliangalie na tuone linasababishwa na nini. Lakini sababu moja kubwa ambayo ninaijua ni umwagikaji wa mafuta yanayotoka kwenye malori ambayo yanapandisha pale polepole na matokeo yake *Diesel* ikimwagika barabarami sote tunajua kwamba barabara itateleza.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kuuliza swalı dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema mara nyingi barabara zinapotengenezwa na baadaye ambapo zinakuwa haziridhishi linakuwa tatizo la Mshauri (*Consultant*). Lakini kwa barabara za Mafia mara nyingi tunalalamika kwamba hawa Makandarasi wanaoletwa Mafia, maisha wanakuwa hawafanyi vizuri kutokana pia na hata usimamizi wa Mkao kuja kusimamia kule. Kwa nini maombi yetu tunayoyaomba kila siku, kuomba kwamba tunaomba tupatiwe sisi wenyewe Halmashauri ya Wilaya ya Mafia magreda ili tuweze kuzisisimamia na kuzikarabati barabara zetu kuititia mfuko wa pesa zinazotoka Wizara yake. Kwa nini mpaka leo Serikali inashindwa kutupatia vifaa hivyo ili tuweze kutengeneza barabara zetu vizuri. (*Makofit*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, tatizo la Mafia ni tatizo maalum. Mafia hakuna udongo na Changarawe ambazo zinaweza kutengeneza barabara ngumu na hilo mara moja ukitangaza *Tender*, Mkandarasi atakuletea tatizo hilo. Kwa hiyo, utengenezaji wa barabara Mafia ni ghali; lakini lazima barabara zitengenezwe. Kwa hiyo, barabara ikishatengenezwa Mafia ni jukumu la Wilaya kukarabati barabara hiyo kila wakati na muhimu sana. Barabara za Mkao ambazo zinatengenezwa Mafia zinakarabatiwa kila wakati, lakini za Wilaya zimekuwa tatizo, na Mafia wameomba mara nyingi tu kununua mitambo yao wenyewe, lakini pesa za Mfuko wa Barabara, ambayo tumepitisha Shera yake hapa haziruhusiwi kutumika kununua mitambo. Ni kukarabati barabara, hiyo ndiyo msimamo wa Sheria inavyosema.

Mheshimiwa Shah amekwishakuja kwangu na nimemshauri Halmashauri ya Mafia ijenge hoja iombe pesa kutoka TAMISEMI ili hoja yao iweze kukubalika kununua mitambo. Nina imani kabisa wamejenga hoja imekwenda na wao wanaifikilia. Lakini msimamo wa Sheria ni huo.

Na. 25

**Makosa ya Ki-Uhamiaji**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED** aliuliza:-

Kwa kuwa ni haki kikatiba na ya kisheria kwamba raia au mtu anayepewa pasi ya ukaazi kujulishwa pindi anapofanya kosa la kiraia:-

- (a) Je, ni raia wangapi waliofanya makosa ya Ki-uhamiaji?
- (b) Je, ni wageni wangapi tangu Januari, 2001 hadi leo wamevunja Sheria za ukaazi?
- (c) Je, ni raia wangapi wamepewa adhabu, na ni adhabu gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Kuteuliwa, lenye sehemu (a), (b) na ( c) kwa pamoja kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, kipindi cha Januari, 2001 hadi Februari, 2005 jumla ya raia wa Tanzania 3,075 wamekamatwa kwa makosa ya kiuhamiaji; kwa mchanganuo ufuataao:-

Mwaka 2001 walikuwa 411, mwaka 2002 walikuwa 922, mwaka 2003 walikuwa 817, mwaka 2004 walikuwa 445 na kati ya Januari hadi Februari, mwaka huu 2005 walikuwa 36. Raia hawa hawa waliofanya makosa ya kiuhamiaji wamechukuliwa hatua za kisheria kama ifuatavyo:-

- Waliohukumiwa vifungo jela ni 307; na
- Waliopewa adhabu ya faini ni 2,581.

Mheshimiwa Spika, kuanzia Januari, 2001 hadi Februari, 2005 jumla ya raia wa nchi za nje waishio nchini 8,652 walivunja Sheria za ukaazi. Mchanganuo wao ni kama ifuatavyo:-

Mwaka 2001 wageni wakaazi 1,410, mwaka 2002 walikuwa 1,768, mwaka 2003 walikuwa 3,573, mwaka 2004 walikuwa 1,445 na kati ya Januari hadi mwezi Februari mwaka huu wageni wakaazi 283. Wamevunja Sheria za ukaazi na wamechukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Uhamaaji Na. 7 ya mwaka 1995.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika nashukuru, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa nchi yetu baadhi ya sehemu zake imezungukwa na Bahari, na kwa kuwa katika sehemu za Bahari kuna tabia ya watu kuingia mara kwa mara kutoka nchi nyingine.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwafuatilia wageni hawa, ili kujua kama kweli wanafuata Sheria au wanavunja Sheria?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika maeneo ya visiwa kama kule Unguja na Pemba, uwezekeno wa wageni kuingia visiwani kuitia majini na hata kukwepa maeneo ya Bandari, wakapita maeneo ambayo hayana Bandari kwa kutumia majahazi huo uwezekano upo sana.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, ndiyo maana katika kukabiliana na tatizo hilo Serikali tunaongeza nguvu ya Idara ya Uhamiaji katika maeneo hayo, ni madogo lakini yote tumeweka Maafisa Uhamiaji, tofauti na Bara ambako kuna Wilaya nyingi sana hazina Maafisa Uhamiaji pamoja na Wilaya yangu ya Manyoni na ziko Wilaya nyingi hazina Maafisa Uhamiaji.

Lakini Visiwani tunaweka wengi kwa sababu ya tatizo hilo la kukabiliana na watu hao na tunaomba vilevile pamoja na Maafisa Uhamiaji nataka nitoe wito kwa raia wazalendo, kila wanapoona wageni ambao wanahisi si wageni ambao wako nchini kihalali basi watoe taarifa kwa vyombo vinavyohusika hasa kwa uhamiaji kwa sababu jukumu hili ni letu sote. (*Makofi*)

Na. 26

### **Uchafuzi wa Hali ya Hewa- Kutokana na Magari.**

**MHE. MARTHA M. WEJJA** aliuliza:-

(a) Je, Serikali inasema nini kuhusu uchafuzi wa hali ya hewa mijini hasa Jiji la Dar es Salaam ambao unaathiri sana afya za wananchi kwa mfano magari mabovu, viwanda na kadhalika?

(b) Je, Serikali inajua kwamba chini ya Sheria ya *Road Traffic*. Na. 114 (i) ina mamlaka ya kuweka viwango vya makelele na moshi kutoka kwenye magari?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Wejja, Mbklunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba moshi mzito wa magari unasababisha uchafuzi wa mazingira na kuathiri afya za wananchi. Kwa kutambua hivyo, Serikali ilitunga Sheria ya Usalama Barabarani Na. 30 ya mwaka 1973, ambayo katika kifungu cha 114 (j), kimeelekeza kuhusu kupunguzwa kwa makelele na moshi wa unaotokana na magari yanayopokuwa barabarani.

Katika kutekeleza Sheria hiyo, Taasisi za Serikali kama vile Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Madini na Nishati, huweka viwango vya bidhaa zinazoingizwa nchini kama vile magari na mafuta yanayotumika kwenye magari na Viwanda. Aidha Shirika la Viwango (*TBS*), limeweka viwango vinavyokubalika vya

magari yanayoingizwa nchini. Hii ni katika kuhakikisha kuwa bidhaa zinazoingizwa hapa nchini zinakuwa katika ubora unaotakiwa ili zisiathiri afya za wananchi.

Vile vile Jeshi la Polisi linaendelea na misako ya mara kwa mara katika kuyakamata magari ambayo hayana viwango vinavyostahili kuwa barabarani na hatimaye kufikishwa katika vyombo vya Sheria.

Aidha hivi sasa Wizara ya Ujenzi inaanadaa muswada wa Sheria kuhusu ukaguzi wa lazima wa magari, yaani (*Compulsory Vehicle Inspection*). Sheria hiyo ikipitishwa, magari yatakayokuwa barabarani ni yale tu ambayo yatakuwa yamekaguliwa na kupata hati ya ubora, na yale magari yanayotoa moshi hayataonekena barabarani.

**MHE. MARTHA M. WEJJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri naomba kuuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Pamoja na kwamba anasema Serikali ina Sheria, na kwamba karibuni Sheria hiyo itatoka. Je, na kwa kuwa nchi yetu ni moja ya nchi zinazoendelea na inapiga vita uchafuzi wa mazingira haioni kwamba sasa muda umefika Sheria aliyosema ni ya magari, haoni kama sasa muda mwafaka umefika kwa viwanda ambavyo vinajengwa bila kujali athari za wananchi, utakuta viwanda vingi vidogo vidogo na vikubwa vinajengwa kwenye makazi ya wananchi. Je, Serikali itachukua hatua gani kuepusha suala hili ili kila wanapojenga wahakikishe wanajenga nje ya makazi ya watu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, aah Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara siyo wa Mambo ya Ndani.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara inakagua kwanza kabla kiwanda hakijajengwa kuna kitu kinaitwa *environmental impact assessment* ambayo lazima kila kiwanda kupita ukaguzi huo kabla hakijasajiliwa na kukubalika kujengwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda ambavyo vinajengwa katika maeneo ya wakazi Serikali imeliona hilo na imepata malalamiko mbalimbali tunalitizama na kulifuatilia na pale ambapo tunaona kuna kiwanda ambacho kimeingilia wakazi Serikali itakuwa tayari kukisimamisha kwa kufuata taratibu zilizowekwa.

Na.27

### **Mradi wa Maji Makondeko**

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA** aliuliza:-

Kwa kuwa mradi wa maji wa Makondeko hapo awali ulikusudiwa kufikisha maji hadi Tarafa yote ya Nanyamba, Kata ya Kiromba na Mnima huko Mtwara Vijiji:-

- (a) Je, kwa nini hadi sasa maji ya mradi huo hayajafika Mtwara Vijijini hasa katika Tarafa ya Nanyamba na Kata ya Mnima na Kiromba?
- (b) Je, Serikali italimaliza lini tatizo hilo ili wananchi wa Nanyamba na Kata ya Kiromba na Mnima waweze kupata maji?
- (c) Je, kwa nini Bodi mpya ya mradi huo wa Maji iliyoundwa hakuna mkazi wa Mtwara Vijijini aliyetoka kama mjumbe katika Bodi hiyo na Serikali itakuwa tayari kuongeza mjumbe mmoja toka Mtwara Vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDDELEO YA MIFUGO alijibu:-**

Mheshimiwa Spika naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Spika Abdillahi Namkulala, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

- (a) Mradi wa maji wa Makonde ambao chanzo chake ni visima virefu vilivyoko kwenye Bonde la Kitangari ulijengwa ili uhudumie pia vijiji vya Namkuku, Dinyech, Chikwaya, Milangominne, Mnyawi, Namtumbuka, Mnongodi, Mnyahi, Mtangani, Mkumbwana na mji mdogo wa Nanyamba. Vijiji hivi vipo katika Tarafa ya Nanyamba, Kata ya Kiromba na Mnima hazikuwa kwenye mpamgo wa kupatiwa maji kutoka kwenye mradi huu. Hata hivyo vijiji vilivyopo katika Kata hizo vitawezakupata maji pale mradi utakapopanuliwa.

Huduma ya maji kwa sasa hivi haipatikani vizuri katika vijiji nilivyovitaja kutokana na matatizo ya uchakavu wa miundo mbinu, ongezeko la watu na upungufu wa umeme wa kuendeshea mitambo. Tatizo jingine ni lile la wananchi wa Tarafa ya Nanyamba kutochangia kikamilifu huduma ya maji inapopatikana.

- (b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na azma yake ya kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma ya maji. Serikali kushirikiana na Serikali ya Japan kuititia *JICA* imeanza mwaka huu 2005 utekelezaji wa miradi ya maji vijiji katika mikoa ya Lindi na Mtwara.

Chini ya mpango huu vijijini vya Mbembaleo, Maranje, Mtiniko na Malamba vilivyoko Tarafa ya Nanyamba vitanufaika. Vijiji vingine vitakavyohudumiwa katika Wilaya ya Mtwara vijijini ni:-

Kitaya, Manyembe- Juu, Nanguruwe, Ziwani, Arusha- Chini Dihimba, Mpondono, Mahurunga, Kitumguli na Kawawa. Serikali itaendelea na juhudi za kuhudumia vijiji vingine katika Wilaya ya Mtwara Vijijini kwa kuzingatia uwezo uliopo vikiwemo vile vya Kata za kiromba na Mnima.

- (c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Bodi ya ya Maji ya mradi wa Makonde haina mjumbe kutoka Mtwara Vijijini. Katika uteuzi wa wajumbe wa Bodi, Wizara huwa inazingatia sana mapendekezo yanayowasilishwa na Wilaya kwa kushirikiana na Mkoa.

Katika uteuzi wa Bodi ya Mradi uliofanyika mwaka 2003, Wilaya ya Mtwara Vijijini, ilichelewa kuwasilisha mapendekezo yake kwa Mkuu wa Mkoa.

Hata hivyo ili kutatua tatizo la uwakilishi na usimamizi wa mradi wa Makonde. Viongozi wa Wizara, Mkoa na Wilaya za Newala, Tandahimba na Mtwara Vijijini walifanya kikao cha pamoja tarehe 10.05. 2005 chini ya uwenyekiti wa Katibu Tawala wa Mkoa, kutafakari mfumo wa uwakilishi katika usimamizi wa mradi.

Aidha, Kamati ya Wataalam iliyokaa tarehe 03.06.2005 imependekeza mifumo ambayo inatarajiwa kuwa shirikishi. Wizara na Mkoa zinafanya uchambuzi mapendekezo hayo ili kuchagua mfumo muafaka kwa ajili ya uendeshaji wa mradi huu.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri, ila nina maswali mawili tu ya nyongeza.

Kwa kuwa wakati tuko kwenye Kamati ya Maji Dar es salaam tulikubaliana vizuri na Mheshimiwa Waziri na alikubali kupeleka Milioni 40, mradi wa Makonde kukarabati na Milioni 10 kukarabati mabomba Nannyamba ili maji ya Makonde yafike Nannyamba, lakini Milioni 10 hizi ni kijiji tu cha Nanyamba; Je, Wizara iko tayari kuhakikisha maji yanafika kijiji cha Nambau kule Tandahimba ili watu wa Nitekela na Njengwa alikotaja wachukulie Nambau?

Swali la pili, kwa kuwa tatizo la Mtwara Vijijini maji ni kubwa mno. Je, Mheshimiwa Waziri atakubali kuacha kidokezo Wizarani pale ili Mungu akinijalia nikirudi mimi Bungeni hapa, nikae na watu wa Mtwara Vijijini kutengeneza *District Water Master Plan* ili niipeleke Wizarani tukae na Waziri tuiangalie vizuri, nikirudi lakini. Tuiangalie vizuri ili kuondoa tatizo hili? (*Kicheko na Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:**  
Mheshimiwa Spika,

**SPIKA:** Tumsikilize Mheshimiwa Naibu Waziri, endelea Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Ni kweli Mheshimiwa Mbunge katika kikao tulichokuwa pamoja kule Dar es salaam, tuliahidi kufanya hivyo na nitamwomba wakati tunauleta Bajeti yetu ya matumizi ya mwaka 2005/2006, asaidie katika kupitisha kwa sababu mradi huo utakuwa umejumuishwa katika Bajeti yetu.

Pili, *Inshallah*, Mungu akimjalia kurudi, nina hakika tutasaidiana kama alivyosema ili tuangalie mpango. (*Kicheko na Makofi*)

Mhehimiwa Spika, nazungumza kwa niaba ya Wizara, kwa hiyo tutasaidiana na mimi, *Inshallah* nikirudi. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Kwa kuwa Tandahimba imetajwa, nampa nafasi Mheshimiwa Abdula Suleiman Lutavi.

**MHE. ABDULA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Mimi ninataka niulize swali moja fupi tu la nyongeza. Kwa vile mradi huu unaotajwa kunufaisha maeneo haya ambayo yalikuwa yanatolewa majibu sasa hivi na Mheshimiwa Naibu Waziri, chanzo chake ni Kitangali kama alivyotaja.

Kwa kuwa tayari tulikuwa tumejenga tamaa kwamba ukarabati wa mitambo kule Kitangali utakuwa umekwisha fanyiwa kazi. Mimi nilikuwa nataka kujua tu kwamba kwa sababu wananchi bado wanasubiri, ule mpango wa kununua na kuzifunga kule mradi wa Kitangali umefikia wapi hadi sasa hivi? Nakushukuru sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyo eleza kwenye jibu la msingi, tumetenga fedha kwa ajili ya kukarabati mradi mzima wa Makonde, lakini maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Mbunge nitaomba labda tukae tuangalie katika hiyo *package* ya marekebisho au matengenezo itahusisha maeneo yapi.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda nitumie fursa hii kuomba Halmashauri zetu za Wilaya kuingiza mipango ya maji kwa Vijiji na maeneo ambayo yako chini yao. Ni Wilaya chache sana zinazingatia hilo ambalo ni kitu cha muhimu sana kwa ajili ya kusaidia wananchi kupata maji. Kwa hiyo nitaomba Wilaya zote waweze kuongeza kasi ya kuipanga mipango ya maji katika Bajeti zao.

Na. 28

### **Tatizo Sugu la Maji Lushoto**

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU** aliuliza:

Kwa kuwa tatizo la maji kwa Mji wa Lushoto linazidi kuongezeka siku hadi siku kutokana na kupungua kwa maji katika vyanzo vilivyopo:-

- (a) Je, Serikali inachukua hatua gani kuondokana na hali hiyo?
- (b) Kuna mkakati gani wa kudumu dhidi ya tatizo hilo?

### **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mbunge wa Lushoto, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwepo na upungufu wa maji kwa Mji wa Lushoto kunakosababishwa na upungufu wa maji kwenye vyanzo

vyake kutokana na ukataji miti hovyo, ufugaji usiozingatia kanuni, kilimo na shughuli zingine zinazoathiri mazingira kwenye vyanzo hivyo

Katika jitihada za kupunguza tatizo la maji katika mji wa Lushoto, Wizara yangu ilitenga shilingi milioni 10 katika kipindi cha mwaka 2003/2004 kwa ajili ya uwekaji wa bomba kuu jipya eneo la Kamfa na ukarabati wa chanzo cha Kwembago.Marekebisho haya yameleta manufaa kwani leo Mji wa Lushoto umeweza kupata maji kwa saa 12 badala ya wastani wa saa 6, kabla ya ukarabati huo.

Aidha, Bodi ya maji Mjini Lushoto imeweka utaratibu wa kuweka akiba ya shilingi 300,000/= kila mwezi kuipa Mamlaka ya Maji Mjini Lushoto uwezo wa kukarabati Miundombinu ya mradi pale inapohitajika ili kufanya mradi kuwa endelevu. Hadi sasa kiasi cha shilingi 11,000,000/= zimekusanya.

- (b) Mheshimiwa Spika, ili kuondoa kabisa tatizo hilo katika mji wa Lushoto, Wizara yangu ikishirikiana na Halmashauri ya Wilaya, imeufanyia mapitio mfumo mzima wa maji ya mji wa Lushoto na kuufanyia usanifu, ambapo kiasi cha shilingi milioni 369 zinahitajika ili kukarabati na hivyo kuwezesha kutoa huduma ya maji kwa wakazi wote wa Lushoto.

Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya, inatafuta Wahisani na vyanzo vingine vya fedha kugharimia mradi huu. Hivyo tunaishauri Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kuona umuhimu wa mradi huu na hivyo kupendekeza katika Bajeti yake ya kila mwaka ili mradi huu uweze kutekelezwa.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, ninafurahi kwa majibu mazuri ya kutia moyo, lakini nina swali moja la nyongeza:-

Kwa kuwa tathmini ya mradi ambaao ameusema Waziri ilikwishafanyika na kianzio cha maji kutoka kianzio cha Kiboco kilipatikana na thamani ya mradi ule ilifikia kama milioni 800. Naibu Waziri alipotembelea Lushoto alikabidhiwa mradi ule na kuahidi kwamba utaingizwa katika miradi ya Benki ya Dunia. Je, ni kweli mradi huo anao na utaingizwa katika miradi ya Benki ya Dunia?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli nilipotembelea huko nilikabidhiwa rasimu ya mradi huo ambaao wataalam wetu wa Wizara wanaifanyia kazi.

Pili, ikiwa fedha za Benki ya Dunia zitakapo kuwa tayari, nina hakika kipaumbele kitawekwa katika mradi huo ambaao uko kwenye Wilaya ya Lushoto.

Mheshimiwa Spika, Vile vile katika kipindi cha mwaka huu wa 2005 wa fedha kutokana na Bajeti yetu, tumetenga fedha shilingi milioni 35 ambazo tutaomba Bunge lako Tukufu kuziidhinisha ili kwenda kusaidia ukarabati wa mradi huu.

### **Ruzuku Kwa Dawa ya Kupulizia Mikorosho**

**MHE. ALHAJI AHAMADI HASSAN MPEME** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imetoa ruzuku kwa mbolea kwa lengo la kuwapunguzia mzigo wakulima ili waweze kuzalisha mazao mengi zaidi wapate faida ya kutosha na kwa kuwa Mkoa wa Mtwara unajishughulisha zaidi na kilimo cha korosho kuliko mazao mengine yoyote na hivyo wanahitaji zaidi dawa za kupulizia mikorosho kuliko mbolea:-

Je, Serikali haioni kuwa ni vizuri kuwasaidia wakulima wa mkoa huo kwa kuwapatia ruzuku kwa dawa za kupulizia mikorosho ili kuwapunguzia mzigo mkubwa wa gharama ya kununua dawa hizo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Hassan Mpeme, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza nilipokuwa najibu swalii Namba 125 la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo katika Mkutano wa 19 wa Bunge, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mpeme na Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inaona kwamba ni vizuri kuwasaidia wakulima wa Mkoa wa Mtwara na Mikoa mingine inayolima mikorosho kwa kuwapatia ruzuku katika dawa ya kupulizia mikorosho ili kuwapunguzia mzigo wa gharama za kununulia dawa hiyo. Kuanzia Mei, 2005, Serikali itatoa ruzuku kwa dawa ya mikorosho isiyokuwa na athari kubwa kwa mazingira kama ifuatavyo:-

Serikali itatoa ruzuku ya fidia asilimia 50 ya bei za kununulia dawa ya mikorosho. Pili, Serikali itatoa ruzuku ya kufidia gharama za usafirishaji wa dawa hizo hadi kwenye vituo vikuu vya kupokelea dawa hizo kwa asilimia mia moja. Vituo hivyo ni Mtwara Mjini, Tunduru Mjini, Lindi Mjini, Tanga na Dar es salaam ambacho kitahudumia Mikoa ya Dar es salaam, Pwani na Morogoro. Tatu, Serikali itatoa ruzuku ya kuyafanya matengenezo mabomba ya kunyunyizia dawa na kuyarekebisha ili yawezesha kutumiwa kunyunyizia dawa ya maji.

**MHE. ALHAJI AHAMADI HASSAN MPEME:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

Kwa kuwa makusudio ya Serikali kuunda mfuko wa pembejeo ni kutaka kuwawezesha wakulima kuzalisha mazao kwa wingi zaidi na kwa ubora zaidi. Sasa, Je, mfuko huo kwa nini mara nyingi sana unakopeshwa wafanyabiashara binafsi kuliko wakulima wenywewe? Swalii ya pili,

**SPIKA:** *Microphone* yako iko mbali, hatukusikii vizuri

**MHE. ALHAJI AHAMADI HASSAN MPEME:** Labda nirudie. Makusudio makubwa kabisa ya kuanzishwa kwa mfuko wa pembejeo ni kuwasaidia wakulima waweze kuzalisha mazao kwa mengi zaidi na yenye ubora mkubwa zaidi. Sasa imekuwaje mfuko huo fedha zake wanakopeshwa wafanyabiashara zaidi kuliko wakulima wenywewe?

Swali la pili, kwa kuwa Mawakala wa uagizaji wa dawa za kupulizia mikorosho ni wafanyabiashara wa Kihindi sana, na kwa kuwa wanapoziagiza dawa hizo huzificha kwa makusudi, hawafikishi mapema kwa wakulima kwa makusudio ya kutaka kuwalangua. Sasa ili wananchi wafaidike na ruzuku ya Serikali:. Je, sasa Serikali haioni umuhimu wa kuwakopeshwa fedha vyama vya Ushirika ili wawe mawakala wa kuagiza dawa hizo ili wakulima wafaidike na ruzuku?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, Kwanza, napenda kumpongeza kwa kufuatilia masuala ya kilimo cha koroshomkatika maeneo husika, hongera sana.

Pili, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-Mfuko wa Pembejeo ulipoundwa, lengo lilikuwa ni hasa ni kuunda uwezo wa *Stockis*, wanalitumia neno *Stockis* ambao wanawenza wakaweka bidhaa kwa wingi sana na kuzisogeza karibu na Mikoa na Wilaya husika. Ndiyo maana wanaokuja pale ni watu wenye uwezo hata wa kuweka rehani. Lakini tukiagiza mkulima mmoja mmoja mdogo mdogo huenda tukapata matatizo kama tulivyopata huko nyuma ya bilioni 5.

Ya pili, Mheshimiwa Spika, naomba kusema hivi, ni kweli ipo sababu ya kuwahusisha vyama vya Ushirika na wengineo kufanya hivyo. Inafanyika hivyo. Kwa hivi ni ruksa vyama vya Ushirika kukopa, pili mifuko ya pembejeo kwa mfano, Tunduru wana mfuko wa pembejeo na wamewahi kukopeshwa. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anaweza kuthibitisha jibu langu. Tat, vile vile *Association* za wakulima ruksa, karibu sana kukopeshwa.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swal la nyongeza. Kwa vile umesema kwamba ruzuku imetolewa tangu Mwezi Mei, 2005 na huu ni Mwezi wa Sita/Juni, 2005. Je, una uhakika hizo fedha zimeshatolewa au ruzuku imeshatolewa kwa kuwa mimi nina ukweli kwamba mpaka hadi sasa wakulima wangu hawajapata *Sulfur* kwa bei hiyo unayoizungumzia kutokana na ruzuku?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, mazungumzo haya yote ninayoyazungumzia yalifanyika naomba kumtaarifu Mheshimiwa Kigwalilo yalifanyika mwezi Machi, mwaka huu. Baada ya kutafiti bei mbali mbali tukakubaliana zitengwe fedha, imetengwa shilingi bilioni moja kwa shughuli hizo. Kwa hiyo *Stockis* karibu. (*Kicheko*)

**Msamaha wa Kodi na Ushuru wa Pembejeo za Kilimo**

**MHE. OMAR S. KWAANGW'** aliuliza:-

Kwa kuwa nia ya Serikali ni kuwawezesha wakulima kutumia zana bora za kilimo ili kuinua mapato yao na Taifa kwa ujumla kama sehemu ya Mkakati wa Kuondoa Umaskini:-

- (a) Je, ni pembejeo na zana zipi za kilimo ambazo zinapata msamaha wa kodi na ushuru mbali mbali na kwa viwango vipi?
- (b) Je, ni kwa kiasi gani Serikali inaweza kusema kuwa misamaha hiyo imewanufaisha wakulima moja kwa moja?
- (c) Kama nia ya Serikali ni kumwezesha mkulima kwa dhati kabisa. Je, ni kwa nini vipuri vya Zana za Kilimo (*spareparts*) zinatozwa kodi ya VAT wakati inafahamika kuwa vipuri ndiyo vifaa muhimu vinavyonunuliwa kila mara kuliko zana zenyewe ambazo mkulima anweza kununua mara moja baada ya miaka mitano hadi kumi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Omar Kwaangw' Mbunge wa Babati Mashariki lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Na. 24 ya mwaka 1997 (*Value Added Tax Act No. 24 of 1997*), pembejeo zote za zana za kilimo zimesamehewa kadi ya ongezeko la thamani na ushuru wa forodha (*zero rated supplies*). Pembejeo zenyewe msamaha huo ni pamoja na mbolea na dawa za kilimo. Zana za kilimo ambazo hazitozwi kodi ni matrekta, plau, haro, mashine za kupandia mbegu, mashine za kuvunia mazao mashambani, mabomba ya kunyonyizia dawa, majembe ya mkono, reki, rato, sururu, mashoka na mapanga.

Misamaha ya kodi na ushuru wa forodha imepunguza bei za kuuzia pembejeo na zana za kilimo kwa asilimia 25: asilimia 20 ikiwa ni kodi ya ongezeko la thamani na asilimia 5 ikiwa ni ushuru wa forodha.

- (b) Mheshimiwa Spika, kuondolewa kwa kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa forodha kumewezesha zana na pembejeo za kilimo kuingizwa nchini kwa wingi na wananchi kuzinunua kwa wingi na kwa bei nafuu. Kwa mfano, matrekta yaliyoingizwa nchini mwaka 1996/1997 yalikuwa 49 tu ikilinganishwa na matrekta 375 yaliyouzwa katika mwaka 2002/2003.

- (c) Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa linalosababisha vipuri vya matrekta na zana za kilimo kutosamehewa kodi ni kuwa baadhi ya vipuri hivyo vinaingiliana na vile vya magari ambavyo hutozwa kodi.

Mamlaka ya Kodi ya Mapato Tanzania na Wizara ya Kilimo na Chakula wanaangalia mfumo na taratibu za kutambua vipuri vya matrekta na vya zana za kilimo vinavyoweza kusamehewa kodi.

Mapendekezo hayo yatakapokuwa tayari, itayafanya kazi kwa lengo la kuwawezesha wakulima kunufaika na msamaha huo bila kutoa mwanya wa kutumika kinyume na lengo lililokusudiwa.

**MHE. OMAR S. KWAANGW'**: Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili madogo: Kwa kuwa katika mfumo wa soko huria zana nnyingi huingizwa nchini zikiwa katika viwango mbali mbali. Sasa, Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwambna vituo vya majaribio katika ngazi ya Wilaya ya zana za kilimo katika kuona ubora wake kama zinfaa kwenye maeneo mbali mbali. Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba kuna hivyo vituo?

Swali la pili, Kwa kuwa Kituo cha kutengeneza zana za kilimo *CAMATEC*, katika miaka ya hivi karibuni kimeonyesha kwamba hakifanyi kazi yake sawa sawa. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba kituo hicho kinafanya kazi zake kama ilivyotazamiwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, Ni kweli vitu huingizwa kwa viwango mbali mbali lakini hivi vifaa vyote vinaingia katika Bandari na vinakaguliwa na wataalam wa kutoka *TRA*, kwa hiyo ufanuzi halisi, nani ataainisha vitu hivyo, ni Maafisa wa *TRA* Dar es salaam au Tanga na kadhalika.

Pili, *CAMATEC*, pamoja na kuwa zinashughulika sana na zana za kilimo, hadi sasa bado hakijakuwa kituo chini ya Wizara ya Kilimo, kinahusu Wizara ya Viwanda na Biashara. Lakini hata hivyo ninapenda kusema kuwa Serikali inakitazama kiwanda hicho kwa namna ya pekee kwa sababu kina uhusiano mzuri sana na uzalishaji wa kilimo nchini.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Sasa tunaendelea na shughuli nyingine. Kwanza, matangazo.

Tangazo la kwanza , ninayo Barua ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kiongozi wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni inayo niarifu kwamba atakuwa safarini Mkoani Kigoma na baadaye nje ya nchi kwa shughuli za kikazi kuanzia tarehe 7 Juni, 2005 hadi tarehe 13 Juni, 2005. Wakati atakapokuwa hayupo, Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Anna Abdallah, ndiye atakayekaimu nafasi ya Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. (*Makofsi*)

La pili Waheshimiwa Wabunge, Muswada ulioko kwenye *Order Paper*, una marekebisho muhimu ambayo yanakamilika kutolewa sasa kwenye mashine za kufytulia karatasi. Ningomba kabla hamjaenda kwenye chai msubiri ili mgawiwe hayo marekebisho ili kusudi muwe nayo mkononi wakati Muswada unawasilishwa. Mwisho wa Matangazo. Katibu tuendelee na *Order Paper*.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### **Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2005 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2005**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa hoja yangu, napenda nichukue nafasi hii kukupongeza wewe kwa siku ya leo kwa sababu ndio *Birthday* yako. Nakutakia afya njema na maisha mrefu. (*Makofii*)

**SPIKA:** *I am over twenty one. (Kicheko)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2005 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2005* sasa usomwe mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho katika Muswada huu ni zifuatazo:-

- (1) Sheria ya Tume ya pamoja ya Fedha ya mwaka 1996 (*The Joints Finance Commission*);
- (2) Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2002 (*The Non Governmental Organisations Act 2002*);
- (3) Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 (*The Land Act, 1999*)
- (4) Sheria ya Shirika la Taifa la Nyumba ya mwaka 1990 (*The National Housing Act 1990*)
- (5) Sheria ya Mahakama za Ardhi ya mwaka 2002 (*The Land Disputes Court Act of 2002*)
- (6) Sheria ya Kudhibiti Kodi ya Pango ya mwaka 1984 (*The Rent Restriction Act 1984*)
- (7) Sheria ya Ununuzi wa Vifaa vya Umma ya mwaka 2004 (*The Public Procurement Act 2004*);

(8) Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ya mwaka 1979 (*The Local Authorities Elections Act 1979*);

(9) Sheria ya Madaktari sura ya 409 ya Sheria za Nchi (*The Medical Practitioners and Dentist Ordinance Cap.409*);

(10) Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa ya mwaka 1999 (*The Political Leaders Retirement Benefits Act 1999*);

(11) Sheria ya Tume ya Huduma za Bunge ya mwaka 1997 (*The Parliamentary Services Commission Act 1997*);

(12) Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria ya mwaka 1980 (*The Law Reform Commission of Tanzania Act 1980*);

(13) Sheria ya mwisho ni Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ya mwaka 1999 (*The National Health Insurance Fund Act 1999*).

Mheshimiwa Spika, Sheria ya kwanza iliyopendekezwa kufanyiwa marekebiso ni Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha.

Madhumuni ya marekebiso hayo ni kumpatia Waziri wa Fedha mamlaka ya kutengeneza kanuni chini ya Sheria hiyo ambazo zitaweka utaratibu wa Sheria wa namna Tume itakavyoweza kutekeleza majukumu yake mbalimbali chini ya Sheria hiyo. Hivi sasa Sheria haimpi Waziri mwenye dhamana ya Tume, yaani Waziri wa Fedha mamlaka hayo. Hali hii isiporekebisha yaweza kukwamisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Tume ambazo haziwezi kutekelezwa kwa ufanisi bila ya kuwa zimefafanuliwa vizuri kupitia kanuni zilizotengezwa chini ya Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya pili inayopendekezwa kufanyiwa marekebiso na Muswada huu ni Sheria ya Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali (*The Non Governmental Organizations Act*) ya mwaka 2002. Katika Sheria hii, vifungu kadhaa vinapendekezwa kufanyiwa marekebiso. Vifungu hivyo ni kifungu cha pili kinachohusu tafsiri ya maneno na jinsi yalivyotumika katika Sheria hiyo. Katika mabadiliko hayo neno *Non Governmental Organization* limefafanuliwa upya. Hivyo, ufanuzi uliokuwepo awali umeondolewa ili kutovihuisha au kuonekana kuvihuisha Vyama vya Diasa, Madhehebu ya Dini, Vyama vya Michezo na Vyama vingine vya hiari katika maudhui ya Sheria hiyo. Aidha, katika mabadiliko ya kifungu hicho, ufanuzi wa neno *non-partisan* umeongezwa katika Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, marekebiso mengine katika Sheria hii yanahu vifungu vya 11, 12, 18, 24, 31 na Jedwali la Sheria hiyo. Mojawapo ya marekebiso ya msingi katika vifungu hivyo yanahu aina za *NGOs* zinazoweza kusajiliwa kama Mashirika ya Kimataifa (*International NGOs*) na pia unawekwa wazi ukomo wa Wajumbe wa Bodi na sababu zinazoweza kusababisha ukomo huo (*sessional of Membership to the Board*)

Mheshimiwa Spika, mapendekezo mengine ya Muswada huu yanalenga katika kuhuisha Sheria za Ardhi hususan Sekta Ndogo ya Maendeleo ya Makazi ili kuondoa matatizo makuu yafuatayo:-

Kwanza, ukiritimba uliopo kwa wenge nyumba katika kudai na kupata kodi ya pango la nyumba kutoka kwa wapangaji;

Pili, kutokuwepo vigezo vilivyo wazi katika kuweka viwango vya kodi ya pango la nyumba na katika kutoa ilani kwa mpangaji asiyezingatia masharti ya Mkataba wa Upangishaji wa Nyumba au Ardhi.

Tatu, Mashirika ya Umma yanayowekeza katika kujenga nyumba za kupangisha kushindwa kudai kodi za pango la nyumba kwa wakati na hivyo kuathiri uwezo wa Mashirika hayo kimtaji unaotegemea kodi ya pango.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa matatizo hayo, Muswada unapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999, Sheria ya Mahakama za Ardhi ya mwaka 2000, Sheria ya Shirika la Taifa la Nyumba ya mwaka 1990 na Sheria ya Kudhibiti Kodi ya Pango la Nyumba ya mwaka 1984. (*Makofisi*)

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kuitia Muswada huu Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 ifanyiwe marekebisho ili kuwianisha (*to harmonize*) matakwa ya Sheria hiyo na yale yaliyopo kwenye Sheria ya Kudhibiti Kodi ya Pango la Nyumba ya mwaka 1984. Marekebisho haya pia yanakusudia kuondoa migongano ya malengo na madhumuni ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 na Sera ya Taifa ya Makazi ya mwaka 2000, inapoelekeza kufuta Sheria hiyo ya Kudhibiti Kodi ya Pango la Nyumba la mwaka 1984.

Hata hivyo, pamoja na pendekozo la kuifuta Sheria hiyo, inapendekezwa kwamba, baadhi ya masuala yaliyomo kwenye Sheria hiyo, yaani hiyo *Rent Restriction Act* sasa yaingizwe kwenye Sheria tatu zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho, yaani Sheria ya Ardhi yenyewe, Sheria ya Mahakama za Ardhi ya mwaka 2000 na Sheria ya Shirika la Taifa la Nyumba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mabadiliko makubwa yaliyotokana na Sera ya Ardhi, kumekuwepo na matatizo mengi ya Kisheria ambayo yanaathiri sana utekelezaji wa Sheria mbalimbali ambazo inapendekezwa kufanyiwa marekebisho. Kwa mfano Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 inamtaka mwenye nyumba kwanza apate kibali cha Mahakama ili kuweza kupata haki zake za Mkataba za kutoka kwa mpangaji asiyelipa kodi au asiyetimiza masharti ya upangaji wa nyumba au ardhi aliyokubali kuikodisha.

Masharti ya Sheria hiyo ni pamoja na kumkataza mwenye nyumba kukamata na kunadi mali za mpangaji aliyegoma kulipa kodi mpaka suala hilo liamuliwe na Mahakama. Msimamo huu wa Sheria unaondoa uwiano sawia wa kimahusiano kati ya mwenye nyumba na mpangaji. Hii ni kwa sababu sharti la kibali cha Mahakama

halimhusu mpangaji anapotaka haki yake ya kutoka kwenye nyumba aliyopanga, anaondoka tu.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ni Sheria ya Mahakama za Ardhi ya mwaka 2002 ambayo imeweka utaratibu unaolitaka Shirika la Taifa la Nyumba kufungua kesi zake dhidi ya wapangaji katika Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi. Katika kutekeleza utataribu huu, kesi zinazofunguliwa kwenye Kanda za Mahakama Kuu hapa nchini inabidi zisubiri ujio wa Majaji kutoka Makao Makuu Dar es Salaam, ambao wanazunguka nchi nzima. Utaratibu huu umesababisha kesi za Shirika kuchukua muda mrefu kusikilizwa. Naamini mtakubaliana na Mheshimiwa Spika na Wabunge kwamba imechangia kuwepo na ongezeko la malimbikizo ya madeni ya kodi ya nyumba.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ni Sheria ya Shirika la Nyumba ya mwaka 1990 ambayo hailiwajibishi Shirika kuijendesha kibiashara. Hii ni kutoptana na dhana ya huko nyuma kuwa Shirika liliundwa kwa ajili ya kutoa huduma na si kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, msimamo huu ni kinyume na maelekezo ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 inayolitaka Shirika lijiendeshe kibiashara.

Mheshimiwa Spika, mfano wa nne ni Sheria ya Kudhibiti Kodi ya Pango ya mwaka 1984 ambayo kwa kiasi kikubwa inamlinda mpangaji dhidi ya mwenye nyumba. Dhana ya Sheria hii inagongana na Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 mafungu ya 77, 88, 89 na 101 ambayo yanaweka mahusiano sawa kati ya mwenye nyumba na mpangaji. Pia, imeelekezwa kuwa Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 itakayosimamia masuala ya upangishaji nyumba, baada ya marekebisho makubwa kufanywa kwenye Sheria ya Kudhibiti Kodi ya Pango ya mwaka 1984 huko nyuma, Serikali inaamini kwamba ipo sababu tena ya kuendelea na Sheria hiyo inayoondoa uwiano bora kati ya mwenye nyumba na mpangaji.

Mheshimiwa Spika, hivyo, katika Sheria nne nilizozotaja Sheria inayofanyiwa marekebisho makubwa ili kukidhi haja iliyoelezwa ni Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999. Inapendekezwa kufanya marekebisho katika vifungu vya 50, 77, 78, 101, 102, 103, 104, 105 na 108 ya Sheria hiyo ili kuboresha mahusiano kati ya mwenye nyumba na mpangaji. Marekebisho haya yanalenga kubadilisha mfumo wa Kisheria uliopo hivi sasa ambao unamtaka mpangaji na mkodishaji wa ardhi au nyumba kutatua au kuondoa tofauti zao za kimkataba kupitia Mahakama. Hivyo, Muswada huu unapendekeza kuondokana na utaratibu wa kupata amri au kibali cha Mahakama. (*Makofi*)

Matumizi ya Mahakama yatakuwa pale tu mwenye nyumba au mpangaji atakapohiari mwenyewe kutumia haki yake ya Kikatiba kudai haki zake. Pia, pale itakapodhihirika kuwepo dalili za uvunjifu wa amani kutoptana mpangaji kugoma au kuzuia juhudzi za mwenye nyumba kuuza mali za mpangaji aliyeshindwa kulipa kodi ya pango la nyumba ili kufidia malimbikizo ya kodi ya pango. (*Makofi*)

Pia, katika marekebisho haya inakusudiwa kuondoa ukiritimba na kuweka misingi ya uwazi ya kupanga na kukadiria viwango vya kodi ya pango kudai kodi ya pango la ardhi na nyumba na kutoa ilani ya kusudio la kufuta mkataba wa pango.

Mheshimiwa Spika, aidha fungu la 50 la Sheria hiyo inapendekezwa lirekebishwe ili Balaza la Ardhi na Nyumba la Wilaya liwe na mamlaka ya kushughulikia madai ya kodi ya pango na madai ya kodi ya pango la ardhi kwenye Wilaya badala ya Mahakama ya Wilaya. Mahakama ya Wilaya itasikiliza tu kesi za ardhi pale ambapo Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya halijaanzishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa lengo hilo, inapendekezwa lianzishwe fungu hilo kwa kuongeza kifungu cha tatu kinachoendeleza dhana ya kifungu cha 2(1)(b) cha Sheria ya Kudhibiti Kodi ya Pango ya mwaka 1984 kinachompa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya ardhi na makazi kutangaza baadhi ya vifungu vya Sheria kuhusiana na masuala ya upangishaji na upangaji visitumike kwa aina ya ardhi au nyumba zitakazoainishwa au kupendekezwa na Waziri.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kufuta kifungu cha kwanza cha fungu 101 ili kumwezesha mwenye nyumba kuvunja Mkataba wa Upangaji kwa kuingia ndani ya nyumba (*re-entry*) au kuchukua nyumba yake kwa utaratibu unaopendekezwa katika Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya marekebisho ya fungu la 102 yanaweka taratibu za kumwezesha mwenye nyumba kukamata mali ya mpangaji na kuiiza ili kupata malimbikizo ya kodi ya pango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, fungu la 106 inapendekezwa lirekebishwe kwa kuongeza kifungu kipycha (1) kinachompa mamlaka Waziri kutengeneza fomu ya kutolea ilani yaani, *notice*.

Aidha, kinafanua taratibu za kutoa ilani mbadala pale mlengwa anapokuwa hapatikani au anapokwepa kupokea ilani hiyo. Inapendekezwa kuwa ilani katika mazingira hayo inaweza kutangazwa au kubandikwa mahali palipoainishwa kwenye kifungu hicho na ilani hiyo yaweza kuwa kwenye lugha ya Kiswahili, Kiingereza au vyote viwili.

Mheshimiwa Spika, fungu la 108 la Sheria hiyo ya ardhi inapendekezwa irekebishwe kwa kuondoa Ibara ya aya kifungu kidogo cha (1) ili kutambua pendekezo la kufutwa kwa Sheria ya Kudhibiti Kodi ya Pango ya mwaka 1984. Hii ni kwa sababu fungu la 25 la Sheria hiyo kwa kiasi kikubwa limepitwa na wakati na pia baadhi ya maudhui ya fungu hilo tayari yameingizwa na vifungu Na.3(1) (j) na (k), kifungu cha 88, 89, 102, 104 na 105 ya Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 pamoja na kifungu cha 56 cha Sheria ya Mahakama za Ardhi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Shirika la Nyumba ya mwaka 1990 inapendekezwa nayo ifanyiwe marekebisho katika vifungu vifuatavyo:- Kifungu cha 2, 4, 11 na 31 ili

kuliwezesha kisheria Shirika la Nyumba kutekeleza majukumu yake kibiashara na kwa ufanisi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, fungu la (2) la Sheria hiyo la Shirika la Nyumba inapendekezwa kuhuisha tafsiri ya baadhi ya maneno ambayo awali yalitafsiriwa kwenye Sheria ya Kudhibiti Kodi ya Pango la Nyumba ya mwaka 1984 ili yaoane na tafsiri zilizomo kwenye Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, ili kuleta dhana ya uwazi katika kuweka viwango vya kodi ya pango, inapendekezwa kurekebisha fungu la 11 la Sheria ya Shirika la Taifa la Nyumba ya mwaka 1990 na fungu la 78 la Sheria ya Ardhi kwa kupendekeza vigezo vya jumla vitakavyozingatiwa katika kuweka au kukadiria kodi ya pango la nyumba inayokodishwa. Vigezo vinavyopendekezwa ni pamoja na kuzingatia ukubwa, matumizi, thamani, mahali na hali ya nyumba inayopangishwa.

Pia, kwa kuzingatia kuwa mwenye nyumba analipa Bima, kodi na ada mbalimbali za kisheria na pia ameingia gharama za matengenezo ya nyumba kwa mujibu wa Mkataba au Sheria na utamaduni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa dhana potofu kwa Shirika la Nyumba la Taifa kwamba ni la kutoa huduma bure, inapendekezwa fungu la (4) lionezewo kifungu kidogo cha (5) kitakacholiwajibisha Shirika kuonekana linatekeleza majukumu na wajibu wake kwa misingi ya kibiashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha fungu la 31 inapendekezwa lirekebishwe kwa kuongeza kifungu kidogo cha (2) cha kuwataka Wajumbe wa Bodi ya chombo hicho na watumishi wa Shirika hilo wawajibike kutangaza mgongano wa maslahi kwenye masuala yanayowahusu wao binafsi au jamaa wa karibu kama inavyoainishwa na fungu la 15 la Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999. Hii itaimarisha utawala bora ndani ya Shirika. Lengo la mapendekezo haya ni kuweka mazingira muafaka ya uwekezaji katika ujenzi wa nyumba za kupangisha bila kuathiri maslahi ya wapangaji na wenyе nyumba.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya mwisho katika marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria nilizotitaja katika sehemu hii inahusu mapendekezo ya kurekebisha kifungu cha 37 cha Sheria ya Mahakama za Ardhi ya mwaka 2002. Muswada unapendekeza marekebisho katika fungu la 37 la Sheria hiyo ili pale ambapo Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi hakijaanza kufanya kazi kutokana na upungufu wa Majaji. Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya lishughulikie migogoro ya ardhi na nyumba inayohusu Mashirika ya Umma yaliyoainishwa chini ya fungu 37 fungu dogo la (1)(d) cha Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Saba inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya ununuzi wa vifaa vya umma ya mwaka 2004. Sheria hii inafanyiwa marekebisho katika vifungu vya 82 na 84 ili kuweka muda unaotosha kuwezesha mlalamikaji na mlalamikiwa kuweza kuwasilisha kumbukumbu muhimu katika Mamlaka ya Rufaa na pia kutoa muda halisi kwa Mamlaka ya Rufaa chini ya Sheria hiyo kuweza kufikia maamuzi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Nane inayopendekeza kurekebisha, kupitia Muswada huu ni Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ya mwaka 1979. Katika mapendekezo hayo, kifungu cha 40 inapendekezwa kifanyiwe marekebisho ili Wagombea Udiwani kabla ya kuteuliwa kwa ajili hiyo watakiwe kutangaza maslahi waliyonayo katika Mikataba kati yao na Halmashauri husika. Ilivyo sasa Sheria inamtaka mhusika kutangaza maslahi yanayohusika ndani ya siku 30 kabla ya tarehe ya Uchaguzi. Hivyo, Msimamizi wa Uchaguzi hana mamlaka ya kukataa kumteuwa Mgombea kwa vile uteuzi wa Mgombea unafanyika zaidi ya siku 30 kabla ya kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya yanawezesha kufahamika mapema wanaostahili kuwa Wagombea na hivyo kuteuliwa. Marekebisho haya vile vile yakikubaliwa na Bunge lako Tukufu, yataepusha uwezekano wa wasiokuwa na sifa kuchaguliwa na baadaye kusababisha matokeo ya uchaguzi kuhojiwa Mahakamani na kutenguliwa kwa sababu hiyo. Marekebisho haya yanakamilisha marekebisho yaliyokusudiwa katika eneo la Sheria hiyo ili kuboresha Sheria za Uchaguzi kabla ya Uchaguzi Mkuu ujao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Sheria ya 9 inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Madaktari (*The Medical Practitioners and Dentists Ordinance*) sura ya 409. Marekebisho katika Sheria hii yanahusu kusamehe Madaktari waliosajiriwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria iliyotungwa Tanzania Zanzibar kulazimika kusajiliwa upya ili waweze kufanya kazi za Uuguzi Tanzania Bara. Pendekeso la pili linahusu kuweka masharti mapya katika Sheria hiyo yatakayowezesha kuwepo kwa kanuni za maadili na taaluma ya Madaktari na kwamba ukiukaji wake utakuwa ni kosa la uvunjaji wa maadili ya taaluma ya Madaktari.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya 10 inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho katika Muswada huu ni Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa ya mwaka 1999. Marekebisho yanayopendekezwa yanatokana na uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa Sheria hiyo pamoja na utekelezaji wa Sheria ya Viongozi wa Kitaifa mwaka 1986 na hitimisho la kazi la viongozi wa kisiasa kwa kuzitumia Sheria hizo kwa pamoja. Hivyo, ili kuweka utaratibu mzuri wa kutekeleza au kulipa mafao ya Viongozi wa Kisiasa Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Siasa ya mwaka 1999 inafanyiwa marekebisho kwa kuainisha aina ya mafao yanayostahili kuwa ndani ya Sheria, yaani *substantive providence* na mafao ambayo yanafaa kuhuishwa baada ya muda maalum kwa kuyaweka katika jedwali la Sheria hiyo na hivyo kuleta unyumbulifu katika utekelezaji wa Sheria hiyo.

Marekebisho mengine ambayo yanategemeana na badiliko hilo yanafafanuliwa katika marekebisho ya vifungu vingine katika Ibara ya 6 ya Muswada ambayo inarekebisha vifungu vya 10, 11, 12, 13 hadi kifungu cha 23. Pia, katika marekebisho haya, Katibu Mkuu wa Hazina na Mheshimiwa Rais kwa vifungu husika anatajwa ndiye *appropriate authority* kwa maana ya Rais kwamba ndio atakuwa anaidhinisha mafao hayo na Katibu Mkuu wa Hazina ndiye mlipaji mkuu wa hayo mafao ya Viongozi wa Kisiasa.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo mengine katika Muswada huu yanahusu kufanya marekebisho katika Sheria ya Tume ya Bunge. Marekebisho yanayopendekezwa ni mwendelezo wa marekebisho niliyoyataja ili kuhuisha mafao na posho za Viongozi wa Kisiasa. Inapendekezwa kuipatia kwa mujibu wa Sheria Tume ya Bunge mamlaka ya kupendekeza kwa Rais viwango vipyta vya posho na mafao ya Wabunge kila baada ya miaka mitano na Mheshimiwa Rais ataamua kama atakavyoona inafaa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Sheria ya 12 inayofanyiwa marekebisho ni sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria ya mwaka 1980. Inapendekezwa kurekebisha kifungu cha sita ili kuongeza idadi ya Makamishna kutoka sita kama ilivyo sasa kuwa tisa ili idadi hiyo iweze kumudu ongezeko la kazi ambazo Tume hiyo inafanya au kutakiwa kufanya kisheria.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya mwisho lakini sio kwa umuhimu, ni Sheria ya Mfuko wa Taifa ya Bima ya Afya ya mwaka 1999. Inapendekezwa kufuta kifungu cha 17 kinachoorodhesha aina ya huduma zisizotolewa na Mfuko wa Bima. Huduma hizo ni pamoja na ununuzi wa miwani kwa wanachama walio na matatizo ya macho.

Kutokana na maombi ya wanachama hasa Walimu kwa Mfuko kuhusu umuhimu wa huduma ya miwani kwa wanachama wenyewe matatizo ya macho na huduma nyingine, inapendekezwa kufuta fungu la 17 ili kutoa fursa kwa Mfuko kuweza kuongeza aina mbalimbali za huduma zitakazotolewa na Mfuko ikiwa ni pamoja na zile ambazo hivi sasa hazitolewi. Hii ni kwa sababu Bodi ya Bima ya Afya imefanya tathmini ya kitaalamu (*actuarial assessment*) na kuridhika kwamba Mfuko unao uwezo wa kutoa huduma muhimu kama vile miwani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, uzoefu umeonyesha kwamba huduma zisizotolewa na Mfuko zinaweza kutolewa pale ambapo kwa kuzingatia uwezo wa Mfuko unaweza kutoa huduma zaidi kwa wanachama wake. Kwa kutambua utaratibu mrefu unaotumika kufanya marekebisho katika vifungu vya sheria Bungeni, inapendekezwa kumpatia Waziri mwenye dhamana ya Afya uwezo wa kuandaa na kutangaza orodha ya huduma ambazo hazitatolewa na Mfuko. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijahitimisha maelezo ya hoja hii, ningependa kuchukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Uongozi wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Athuman Janguo, Mbunge wa Kisarawe, kwa uchambuzi wa kina ilioufanya na hatimaye kuwezesha Muswada huu kuwasilishwa mbele ya Bunge lako asubuhi hii. Serikali inawashukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kisha liupitishe Muswada huu muhimu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofî*)

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO – MWENYEKITI KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Spika, *happy birthday!*

**SPIKA:** *Thank you. (Kicheko)*

**MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO – MWENYEKITI KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Awali ya yote, napenda nichukue fursa hii kutoa salamu za rambirambi kwa wananchi wa Jimbo la Kilombero kutokana na msiba wa ghafla wa Marehemu Abu Towegale Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kilombero. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema Peponi, Amin.

Mheshimiwa Spika, pili, nachukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa Chalinze, Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu na Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi, kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi kuwa Mgombea wa Kiti cha Urais kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofit*)

Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein, Makamu wa Rais wa Serikali ya Awamu ya Tatu na Mjumbe wa Halmashauri Kuu na Kamati Kuu ya CCM kwa kuteuliwa kuwa Mgombea mwenza wa Mheshimiwa Kikwete. Vile vile, napenda kumpongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais wa Serikali ya Mapinduzi wa Zanzibar hivi sasa na Makamu Mwenyeiki wa CCM Zanzibar na Mjumbe wa Halmashauri Kuu na Kamati Kuu ya CCM kwa kuteuliwa kuwa Mgombea wa Kiti cha Urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kwa Mkutano huu, pamoja na kazi nyinginezo ulipatia Kamati yangu kazi ya kuufikiria Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria mbalimbali Na.2 kwa mwaka 2005. Kazi hii ilitekelezwa vyema katika Vikao vilivyofanyika Dar es Salaam na Dodoma tarehe 3 na 6 Juni, 2005.

Aidha, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali juu ya kusudio la kuleta marekebisho katika sheria zilizokusudiwa ambayo yaliwasilishwa na Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kama alivyosema mtoa hoja, Muswada huu unahusu sheria zifuatazo, Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha ya mwaka 1996; Sheria ya Mashirika Yasiyokuwa ya Serikali ya mwaka 2002; Sheria ya Kudhibiti Kodi ya Pango na Nyumba ya mwaka 1984; Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999; Sheria ya Mahakama za Ardhi ya mwaka 2000; Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa ya mwaka 1990; Sheria ya Ununuzi wa Vifaa vya Umma ya mwaka 2004; Sheria ya Uchaguzi wa Madiwani ya mwaka 1979; Sheria ya Madaktari, Sura ya 409; Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa ya mwaka 1999; Sheria ya Tume ya Huduma za Bunge ya mwaka 1997 na Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria ya mwaka 1980.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, kwa mujibu wa Kanuni Na.70(2), Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, sasa naomba kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati nikianzia na yale ya jumla yaliyojitokeza kwenye Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya hadi sasa bado sijayaona marekebisho yaliyoletwa hivi karibuni na kama ulivyo sema mwenyewe kwamba yalikuwa bado yanachapwa, lakini nimemsikiliza vizuri sana Mtoa Mada na mengi yaliyokuwa katika marekebisho hayo ni yale ambayo yametokana na maoni ya Kamati. (*Makofii*)

Sasa kimsingi, Kamati inaafikiana na mapendekezo yaliyokusudiwa takribani katika sheria zote. Hata hivyo, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri katika maeneo kadhaa ya sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali, Kamati inashauri kuwa siku zijazo Serikali ije na marekebisho Bungeni yatakayowawezesha wananchi kushirikishwa kikamilifu katika asasi zisizokuwa za Kiserikali hususani zile za Kimataifa kwa maslahi ya Taifa letu.

Pili, Serikali ilete marekebisho yatakayoongeza majukumu ya Bodi ili kuifanya iwe na mamlaka ya kuhakikisha Asasi hizo zinawafikia wananchi wa maeneo mengine badala ya mtindo uliopo wa sasa wa wamiliki wa Asasi hizo kuchagua maeneo wanayoyataka wao.

Mheshimiwa Spika, katika sheria zifuatazo ambazo zinashughulikia masuala ya upangishaji, yaani Sheria ya Ardhi; Sheria ya Kudhibiti Kodi ya Pango la Nyumba; Sheria ya Mahakama ya Ardhi na Sheria ya Shirika la Nyuma ya Taifa, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(a) Inashauri kuwa sheria zizingatie haki za pande zote zinazohusika na upangaji wa nyumba, yaani mpangaji na mwenye nyumba bila ya kuupendelea upande mmoja.

(b) Kwa kuwa malengo ya kimsingi katika pango la nyumba yanafanana kati ya nyumba za kuishi na kibiashara, Kamati inapendekeza kuwa sheria isizitofautishe. Hii inatokana na uzoefu kuwa katika siku zilizopita nyumba zilikuwa chache na hazikuwa na mwelekeo wa kibiashara na wenye nyumba wengi hawakutegemea nyumba kama chanzo cha mapato yao.

Ni katika kipindi hicho pia sheria zilimlinda sana mpangaji lakini kwa sasa hali ni tofauti, nyumba nyingi zimekuwa ni sehemu ya uwekezaji wa biashara. Kwa mantiki hiyo, kuweka usawa kwa pande zote kutawezesha wapangaji wajione wana wajibu wa kulipa kodi kwa wakati unaostahili na kuchukuliwa hatua wasipotekeleza wajibu wao.

Vivyo hivyo, kuwawezesha wenye nyumba kujipatia vipato vyao bila ya bughudha. Hali kadhalika, marekebisho hayo yatawafanya wenye nyumba kutekeleza

wajibu wao kwa wapangaji kufuatana na mabadiliko ya wakati na kuzingatia mikataba waliyowekeana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu marekebisho katika Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa, Kamati yangu inakubaliana na mapendekezo ya Serikali. Kamati pia inaipongeza Serikali kuitia Mtoa Mada kwa kuzingatia maoni ya Wanakamati ambayo yameufanya Muswada huu uletwe katika sura inayoonekana hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali, Kamati yangu inaafikiana na mapendekezo mengi ya Serikali. Hivyo, Kamati haioni sababu ya kutounga mkono Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii muhimu ya kuwasilisha maoni ya Kamati. Pia, napenda nimshukuru Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mheshimiwa Gideon Cheyo, Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi na wataalam wao kwa ushirikiano mkubwa waliota wakati wa kujadili Muswada huu. (*Makofi*)

Shukrani za pekee ziwaendee Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu kwa kazi nzuri waliyoifanya na kutumia busara ya hali ya juu wakati wa kuuchambua Muswada huu. Mawazo yao mazuri yametuwezesha kuishauri Serikali kama nilivyoeleza hapo awali na naomba niwatambue kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Athumani Janguo - Mwenyekiti; Mheshimiwa George Malima Lubeleje - Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru; Mheshimiwa Grace Kiwelu; Mheshimiwa Rosemary Nyerere; Mheshimiwa Zahor Juma Khamis; Mheshimiwa Khamis Salum Ali; Mheshimiwa Ramadhan H. Khalifani; Mheshimiwa Juma S. N'hunga; Mheshimiwa Ruth B. Msafiri; Mheshimiwa Paschal Degera; Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte; Mheshimiwa Chifu Abdallah S. Fundikira; Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa; Mheshimiwa Jenista Mhagama; Mheshimiwa Mwanne Mcemba; Mheshimiwa George F. Mlawa; Mheshimiwa Raynald Mrope; Mheshimiwa Shoka Khamis Juma; Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe; Mheshimiwa Dr. Nimrod Mkono; Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare. (*Makofi*)

Mwisho kabisa, napenda niwashukuru Ndugu Athumani Hussein, Charles Mloka na Ernest Zulu, Makatibu wa Kamati hii chini ya uongozi thabiti wa Bwana Damian Foka kwa kuihudumia Kamati yetu vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, natamka kuwa naunga mkono Muswada huu na naomba kuwasilisha. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mutungerehi, awasilishe maoni ya Kambi hiyo. Kabla hujafanya hivyo, napenda kuwaarifu kwamba tumepanga kwamba Muswada huu umalizike ifikapo saa saba leo kwa sababu mchana wa leo hatuna Bunge na tutakapokutana tena kesho tunaanza mjadala

wa bajeti. Maombi niliyokwishapokea naona yanatosha kutuwezesha kumaliza Muswada ifikapo saa saba. Nina Wasemaji sita nao ni Mheshimiwa Eliachim Simpassa, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Sophia Simba na Mheshimiwa Semindu Pawa. Basi, mjiandae kuitwa kwa mpangilio huo na naomba tuseme kwa kifupi vile vile ili tuweze kuingia kwenye Kamati ya Bunge Zima kupitisha vifungu vyote. Mheshimiwa Mutungirehi!

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA (MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI k.n.y. MHE. DR. WILLBROD P. SLAA):** Mheshimiwa Spika, saa sita usiku na dakika moja nilikupigia simu nikikupongeza kwa *birthday* yako, kwa hiyo sikupongezi kwa mara nyingine. (*Kicheko*)

Mheshimiwia Spika, napenda nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Wizara hii, Mbunge Shupavu wa Jimbo la Karatu Mheshimiwa Dr. Wilbroad Slaa, kuhusu Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria mbalimbali wa Mwaka 2005 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments (No.2) Bill, 2005*.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea kutoa maoni haya, naomba nitoe pole na salaam za rambirambi kwa familia ya Mheshimiwa Hayati Abu Kiwanga, Mbunge wa Kilombero aliyetutoka juma lililopita. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema Peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Spika, mwaka huu ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu, Vyama mbalimbali vya siasa vimeshawapitisha Wagombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuitia Vyama vyao. Kwa ajili hiyo, napenda niwapongeze Mheshimiwa Augustine L. Mrema, kwa kuitishwa na Mkutano Mkuu wa *TLP* kuwa Mgombea Urais, Mheshimiwa Prof. Ibrahim Lipumba, aliyeteuliwa na Chama cha Wananchi (*CUF*), Mheshimiwa John M. Cheyo aliyeteuliwa na Chama cha *UDP* na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, aliyepitishwa kwa kishindo na Chama cha Mapinduzi (*CCM*). (*Makof*)

Ninawataenia mafanikio mema katika uchaguzi ujao na ikumbukwe kuwa Mwenyezi Mungu anasema katika Qurani Tukufu kuwa: “Huumba nipayo; na humtawaza nimpendaye”. Wale wanaosoma Biblia wanaweza kusoma Yoshua 1:1-9. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Spika, Muswada ulioko mbele yetu unapendekeza marekebisho katika sheria kumi na tatu:-

- (1) *The Joint Finance Commission Act, 1996;*
- (2) *The NGO Act 2002;*
- (3) *The Land Act 1999;*
- (4) *The National Housing Act, 1990;*
- (5) *The Rent Restriction Act, 1984;*
- (6) *The Land Disputes Courts Act 2002;*

- (7) *The Procurement Act 2004;*
- (8) *The Local Authorities Elections Act 1979;*
- (9) *The Medical Practitioners and Dentists Ordinance, Cap.402;*
- (10) *The Political Leaders Retirement Benefits Act, 1999;*
- (11) *The Parliamentary Service Commission Act, 1997;*
- (12) *The Law Reform Commission of Tanzania Act, 1980; na*
- (13) *The National Health Insurance Fund, 1999.*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika baadhi ya sheria zinazofanyiwa marekebisho na sehemu zinazorekebishwa ni chache sana na marekebisho hayo ni ya msingi, Kambi ya Upinzani inayakubali marekebisho hayo kama yalivyoletwa na Serikali. Sheria hizo ni:-

- (1) *The Joint Finance Commission Act, 1996;*
- (2) *The National Housing Act 1990;*
- (3) *The Rent Restriction Act 1984;*
- (4) *The Procurement Act 2004;*
- (5) *The Local Authorities Elections Act 1979; na*
- (6) *The Medical Practitioners and Dentists Ordinance, Cap. 402*

Hizo ni sheria ambazo tunaunga mkono na hatuna hoja na yale yaliyotolewa, lakini katika sheria zifuatazo zinazorekebishwa za:-

- (1) *The Land Act 1999;*
- (2) *The Lands Disputes Courts Act 2002; na*
- (3) *The NGO Act 2002.*

Kambi ya Upinzani inayo maoni yafuatayo kwa kila sheria na marekebisho yake. Kambi ya Upinzani inakubaliana na marekebisho yanayopendekezwa katika kifungu cha 50(1) ili kutoa nafasi kwa mashauri yanayohusu ardhi kufanyika katika Mahakama za Wilaya za kawaida, ambako Mahakama za Ardhi hazijafunguliwa, kwani katika sehemu nyingi za nchi yetu bado Mahakama za Ardhi hazijafunguliwa Wilayani na kulikuwa kunatoka usumbufu mkubwa sana kwa wananchi waliokuwa wakifungua mashauri yanayohusu ardhi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukubali marekebisho hayo, Kambi ya Upinzani ina maoni yafuatayo:-

- (1) Serikali ihakikishe Mahakama za Wilaya zinao Mahakimu wa kutosha na ikiwezekana mmoja ashughulikie mashauri ya ardhi tu.
- (2) Serikali itoe angalau gari moja zuri na fedha za kutosha kuliendesha kwa kila Mahakama ya Wilaya ili kama Hakimu anataka kutembelea ardhi yenyе mzozo aweze kufika huko, kwani mara nyingi wananchi wengi ambao wanakuwa wamedhulumiwa ardhi zao kama hawana fedha za kukodisha magari kwa ajili ya usafiri wa Hakimu na Wazee wa Baraza hupoteza haki zao.

Mheshimiwa Spika, pendekezo hili linawezekana kwani tunaona katika Wilaya, Polisi wanakuwa na magari na wanaweza kufika katika matukio ambayo yametokea huko.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inakubaliana na marekebisho yanayopendekezwa katika vifungu vya 77, 78. Lakini Kambi ya Upinzani haikubaliani na marekebisho yanayofanyika katika kifungu cha 102. Katika vifungu vidogo vya (1)(b) na (3) ambako kuna maneno *Commercial Premises*, tunaomba sheria hii izipe uzito sawa majengo ya biashara na yale majengo ya makazi ya watu kwa sababu mtu anapojenga nyumba ili kupangisha iwe kwa ajili ya makazi ya watu au biashara, anafanya hivyo katika jitihada za kuwekeza ili ajipatie pato.

Tunaishauri Serikali iandae mikakati ya kuwaelimisha wapangaji katika nyumba za makazi kuwa, kulipa pango la nyumba si vibaya kwani, kama wananchi wenyewe uwezo wataona nyumba za kupangisha zinalipa, basi, wawekezaji wa ndani na nje watawekeza katika nyumba za kupangisha na zikiwa nyingi ni dhahiri yafuatayo yatajitokeza.

- (a) Kutakuwa na ushindani;
- (b) Nyumba zitakuwa nyingi na za kutosha;
- (c) Bei za pango zitapungua;
- (d) Mwenye nyumba inayovutia ndiye atapata wateja wengi; na
- (e) Kutakuwa na maelewano kati ya mwenye nyumba na mpangaji.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inayo maoni ya jumla pia katika masuala yanayohusu Sheria ya Ardhi (*The Land Act 1999*) na ile ya Sheria ya Ardhi ya Kijiji (*The Village Land Act No. 5 1999*).

- (1) Tunapendekeza sheria hizi zipelekwe katika kila Ofisi ya Kijiji na Kata, kwani sasa Kata au Vijiji hazina sheria hizo.
- (2) Kila Kijiji kupitia Halmashauri ya Kijiji na Mkutano Mkuu wa Wanakijiji wapewe maelezo juu ya yaliyomo katika sheria hizo na waelekezwe zinakoweza kupatikana.
- (3) Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi itenye bajeti ya kutosha ili kuajiri Maafisa Ardhi wa kutosha kila Wilaya na fedha kwa ajili ya kupima ardhi na mashamba ya wananchi huko vijijini.
- (4) Serikali iwahamasishe wananchi kupima ardhi na mashamba yao.

Tunapendekeza hivyo kwa sababu, kama alivyokwishesema Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, kuwa ardhi ni jambo muhimu katika yale mambo manne kwa maendeleo ya mtu, watu na nchi, vile vile kwa kuzingatia mabadiliko yanayoletwa na utandawazi, mtu akipima ardhi yake au shamba lake na akapewa hati ya kulimiliki atapata faida zifuatazo:-

- (1) Atatumia hati ya ardhi au shamba kupata mkopo kutoka mabenki na vyombo vya fedha. Hivyo, uzalishaji utaongezeka na umaskini utapungua na *MKUKUTA* itakamilishwa.
- (2) Wale wanaotaka dhamana kwa wanafunzi wanaokwenda Vyuo Vikuu watakuwa na cha kuonyesha.
- (3) Mashauri ya ardhi katika Mahakama yatapungua.  
Mheshimiwa Spika, ili kupata fedha za kutosha katika bajeti ya Serikali katika upimaji wa ardhi, yafuatayo yanaweza kufanyika:-

  - (a) Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Ardhi;
  - (b) Kuweka sheria itakayolazimisha angalau asilimia 10 ya kodi inayotokana na watu kumiliki ardhi, viwanja na majengo kuwekwa katika Mfuko wa Ardhi;
  - (c) Kiasi cha fedha zinazolipwa na wamiliki wa ardhi, viwanja na mashamba kuwekwa katika Mfuko huo;
  - (d) Michango kutoka kwa wananchi wengine na hii inawezekana kwa sababu wengine wanachangia harusi na pia Mwenyekiti wa Chama fulani anapochangisha fedha za kufuta Vyama vya Upinzani katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mahakama za Ardhi ya mwaka 2002 ambayo inafanyiwa marekebisho ili Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya kusuluhisha migogoro ya ardhi na Mashirika ya Umma katika kipindi ambacho Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi hakijaanza kufanya kazi kama ilivyokusudiwa. Kambi ya Upinzani inakubaliana na marekebisho hayo, lakini tunayo maoni yafuatayo:

Kwanza, Serikali itenye fedha za kutosha kwa Mhimili wa Mahakama, kwa ajili ya kupata Mahakimu wa kutosha na vifaa vya kutosha vya kufanyia kazi.

Pili, ikiwezekana, ili kupata fedha za kutosha kwa Mhimili wa Mahakama nchini, Bunge litunge Sheria inayolazimisha Serikali kupanga Bajeti kwa uwiano maalum kwa Mhimili yote mitatu, yaani Serikali, Mahakama na Bunge. Kwa mfano 2:3:95 yaani 2% ya Bajeti ya Serikali wapewe Mhimili wa Bunge, 3% ya Bajeti ya Serikali wapewe Mhimili wa Mahakama na 95% ya Bajeti wapewe Mhimili wa Serikali kwa ajili ya shughuli zake na zile za maendeleo.

Maana haiingii akilini pale ambapo, kila Kijiji kinaye Afisa Mtendaji wa Kijiji, kila Kata Afisa Mtendaji wa Kata, kila Tarafa Katibu Tarafa, halafu Tarafa moja yenye Mahakama za Mwanzo nne Hakimu mmoja au Mahakama ya Wilaya yenye Mahakama

za Mwanzo 15 kuhudumiwa na Hakimu mmoja na mahali pengine Vijiji, Kata, Wilaya zina Ofisi lakini hakuna Ofisi za Mahakama na Mahakimu hawana nyumba na wala vifaa vya kutendea kazi.

Mheshimiwa Spika, hali hii inaonyesha kwamba dola kwa maana ya Serikali (*Executive*) wanajipendelea dhidi ya mihimili mingine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu marekebisho ya Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa ya Mwaka 1999, katika Sehemu ya 12, tunapendekeza mpangilio wa madaraja matatu, yaani Spika, Naibu Spika, Wabunge, ubadilishwe na kuwa madaraja manne, yaani Spika, Naibu Spika, Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Wabunge.

Mheshimiwa Spika, nadhani Mwanasheria Mkuu wa Serikali ananisikiliza kwa sababu hata mlivyopanga mshahara mnaelewa ninyi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, ina wasiwasi na nia ya Serikali katika kufanya marekebisho katika Sheria ya Mashirika au Asasi zisizokuwa za Kiserikali (*The Non-Governmental Organization Act, 2002*). Maneno “*non-partisan*” katika tafsiri (*definition*) ya maneno katika sheria yanayosomeka: “*Non-partisan means for the purpose of this Act, means not seeking political power or campaigning for any political party.*”

Sheria hii inakusudia kuviuva Vyama vya Siasa ambavyo havina misingi imara kama CCM. Kwani Vyama vya Siasa hasa vya Upinzani vitazuiwa kuunda NGOs kwa ajili ya kufanya utafiti wa shughuli zake na kutoa mafunzo kwa Viongozi na wanachama na kadhalika.

Ikumbukwe kuwa hapa Tanzania kuna Mashirika ya Kimataifa yasiyo ya Kiserikali yanatoa Misaada ya Kifedha kwa Vyama vya Siasa na Chama Tawala na vile vya Upinzani. Mfano *Institute for Multiparty Democracy*(IMD) ya Uhlanzi; *Friedrich Nauman Foundation* (FNF) ya Ujerumani ambao wanashughulikia kukuza na kueneza siasa za Kiliberali au mlengo wa kati ambao wamekwishatoa mamilioni ya fedha kwa Vyama vyenye Wabunge Bungeni. Iweje Serikali izuie uanzishwaji wa Asasi kama hizo hapa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, marekebisho yanayofanyika katika kifungu cha 11 na kuongeza kipengele kipyta (2) kinachosomeka:- “*Non-Governmental Organization registered or established pursuant to the provisions of any other written law shall be required to apply to the Registrar for a Certificate of Compliance.*” Kambi ya Upinzani inapinga utoaji wa *Certificate of Compliance*, kwani utaratibu huu una lengo la kuingilia shughuli za Mashirika hayo yasiyokuwa ya Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa Marekebisho ya Sheria hii ya *The Non-Governmental Act, 2002*, yanafanyika chini ya Hati ya Dharura, na wadau toka katika NGOs, hawakupata muda wa kuyasoma na kuyatolea maoni. Hivyo, tunashauri

marekebisho hayo yaondolewe katika mjadala wa leo na yawasilishwe kwa wadau kwanza, kwani hakuna sababu za msingi za kuyaleta chini ya Hati ya Dharura.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**SPIKA:** Unawasilisha maoni ya Kambi yako ya Upinzani na sio kutoa hoja. (*Kicheko*)

Sasa namwita Msemaji wa kwanza na naomba kweli tusitumie dakika zote kumi na tano ili tuwe na muda wa kwenda kwenye Kamati ya Bunge Zima. Mheshimiwa Simpasa na Mheshimiwa Shellukindo jiandae.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Napenda kutoa salamu za rambirambi kwa wanachi wa Kilombero kwa kumpoteza Mbunge wao, Mheshimiwa Abu Kiwanga.

Vile vile niwapongeze sana Wagombea wote waliopitishwa na Vyama vyao kugombea nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hususan Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kama Mgombea wetu kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi na Mgombea mwenza Dr. Ali Mohammed Shein, pamoja na Mgombea wa Zanzibar Mheshimiwa Amani Karume. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nitachangia kipande kimoja tu kwenye Sheria ile ya Ardhi. Mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, tumeshirikiana vizuri sana na Mheshimiwa Janguo na Kamati yake pamoja na Mwanasheria Mkuu.

Ninayo machache ya kuzungumza. Kwanza, kama alivyosema Mwenyekiti mwenzangu, kama haya marekebisho wamezingatia kama tulivyokubaliana, naunga mkono hoja lakini kama yatakuja namna nyingine, basi tutatafuta nafasi nyingine ya kuendelea kutafuta haki kwa wapangishaji na wapangaji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, suala la upangishaji wa nyumba, sisi kama Kamati tulipokuwa tumeingia kwenye Kamati ile, tuligundua kwamba *National Housing* walikuwa wanadai wapangaji wao Shilingi biliioni 11. Shirika hili ndilo ambalo linatakiwa kwanza kujiendesha kibiashara kwa sababu Serikali haitoi ruzuku kwa Shirika hili. Lakini pili, vile vile wanatakiwa wajenge nyumba nyingi sana katika Miji yote ili wananchi waweze kupata mahali pa kupanga na vile vile waweze kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa sheria ilivyokuwa bila kufanya marekebisho haya, wawekezaji wengi walishindwa kuwekeza tukawa tunafanya kazi ambayo hata Shirika lenyewe haliwezi kuendelea na hali kadhalika lilishindwa kuhudumia nyumba zake kwa sababu sheria ilivyobana na madeni yalikuwa makubwa walikuwa hawawezi kufanya *maintanance* ya nyumba zao. Kamati yangu imezingatia hilo na katika ripoti, tumetoa hapa mara nyingi.

Lakini baadaye tume pata msukumo mkubwa sana wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilikuwa ni mwezi wa Tatu au wa Pili ambapo aliniagiza mimi mbele ya hadhara kwamba Kamati yako ihakikishe hiyo sheria ya kulinda baadhi ya watu tu ni ya kiunyonyaji, ni lazima sasa ibadilishwe na akaomba aisaini kabla yeye mwenyewe Rais hajaondoka na aliniambia hivyo mwenyewe. Vyombo vya Habari vilitangaza na watu walituona tukiongea naye.

Mimi nilimhakikishia kwamba Mheshimiwa Rais wetu na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, hilo kwa mujibu wa taratibu zetu na sera zetu litatakelezwa. Kwa hiyo, nataka niipongeze Serikali kwa kuwa jambo hilo sasa limeletwa hapa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sheria hii ambayo sasa inarekebishwa mimi nilikuwa nimeng'ang'na na kifungu cha 101 na 102, 101 inaongea juu ya iliyokuwa katika Muswada katika marekebisho ya kwanza haikuwemo lakini tumesema ni vizuri iwemo kwa sababu hiyo inamkataza mwenye nyumba asifanye lolote, mwenye mali hiyo asifanye lolote hata kama mtu yumo ndani au hayumo lakini asifanye lolote kazi yake ni kwenda mahakamani na kurudi, kwenda mahakamani na kurudi kwa hiyo haki yake ya huyo ilikuwa sasa haipo kama tunarekebisha hivyo kwamba kifungu 101 sasa kinaondolewa na kwa hiyo mwenye nyumba ana haki basi mimi nakubaliana na hapo naunga mkono.

Mheshimiwa Spika, lakini kingine ambacho katika marekebisho yale ni 102 ambacho kinatambua tu mambo ya nyumba za biashara, sisi tumesema ni nyumba zote kwa sababu sasa hivi ulimwengu wa leo uwekezaji ni katika vitu vingi, mwengine anawekeza aidha kwenye *transport*, kwenye usafiri tu mabasi. Ukiingia kwenye basi unalipa nauli uwe maskini usiwe maskini utalipa nauli ndiyo mkataba, ndiyo mkataba wewe ulikuwa unaingia kwenye basi mgonjwa au nini mkataba ulipe nauli wengine wamewekeza kwenye *mining*, kwenye migodi unachimba unaauza, wengine kwenye *super market*, ukiingia kwenye *super market* ukinunua vitu ukienda kule kwa *cashier* itabidi ulipe huwezi kusema kwamba kwanza kule kwangu kuna wagonjwa sijui kuna nini hiyo habari haipo duniani ni lazima ulipe pale. Hakuna namna hiyo ni uwekezaji ni biashara na wengine wameamua kwa sasa kuwekeza katika nyumba, mtu anajikusulu yeye na familia yake wajenge nyumba yao wapangishe mtu akae mle ndani huo ndiyo mtaji wao, hayo ndiyo maisha yao mke na watoto.

Mheshimiwa Spika, ifike mahali mtu amepanga mle ndani halipi kodi ukidai hupati chochote hata ukimwambia basi tumeshindwana mkataba umevunja naomba uondoke nataka nipangishe mtu mwengine huwezi kufanya hivyo halafu hata kama akiacha tu apigilie milango yote huwezi kuvunja aah! Hii biashara ya wapi? Kwa sababu sasa ni utandawazi na ni biashara huria ama unalipa ama unaondoka kwa sababu huwezi mimi nikajinyima na wengi wamejenga hapa, kujenga na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika umejenga, umejenga nyumba nzuri tunakupongeza umetutia heshima sana katika eneo lili sasa gharama ile uliyoifanya pamoja na Mama Anna Abdallah na vijana ni kazi ngumu sana, sasa mtu mwengine aje akae tu sheria inamlinda, ukitaka wewe kuchukua nyumba hataki unasema basi naomba basi nikuhamishie mahali fulani hataki, naomba basi niendeleze niikuze hataki na sasa hivi kuna hii *mortgage* kwamba unaweza kuweka

nyumba reheni sasa huwezi kuweka rehani hataki sasa unamkomboaje, MKUKUTA wenyewe unakwenda namna gani? Maana huu ni uwekezaji kama vile wa mabasi kama vile vile wa *super market*, kama vilevile wa *mining*, kama vile kuingia dukani na kununua kitu. Ni lazima, *there should be new thinking and new doing*, huwezi kusema tu ilikuwa ni ya zamani tuliambiwa ni huduma, hakuna huduma hili shirika ni lazima lijiendeshe kibashara, mimi nina nyumba yangu nataka nijikomboe kwenye nyumba yangu kwa hiyo, tunasema ni lazima hayo marekebisho yanachukua nyumba za biashara na nyumba za mtu binafsi.

Katika hiyo naunga mkono, lakini bila hilo siungi mkono kwa sababu hatujapata marekebisho hapa tutakuja kuona lakini wamesoma vizuri nadhani Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kama ipo hiyo mkono tunaunga moja kwa moja. Kama haipo mimi nitaendelea kudai haki ya mwenye nyumba hawezi kujengea mtu akae tu, haiwezekani.

Naunga hoja mkono, ahsante sana.(*Makofi*)

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu kidogo, kabla ya hapo napenda kutoa pole zangu nyingi sana kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga. Alikuwa kwenye Kamati ya Uwekezaji na Biashara ambayo mimi nilikuwa Mwenyekiti wake. Alikuwa na michango mizuri sana, Kamati yangu inamkosa sana. Mungu aiweke mahali pema roho ya marehemu. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mteuliwa wa kugombea Urais kwa tiketi ya CCM Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa uteuzi huo. Mimi napenda kuongeza tu kwamba Rais bora atatoka CCM na Rais bora zaidi atatoka katika Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina mchango katika maeneo machache tu. Katika sehemu ya pili inayohusu Tume ya Pamoja ya Fedha ya Muungano. Kwa bahati nzuri nimehusika na marekebisho haya. Sheria Na. 14 ya mwaka 1996 inahitaji marekebisho zaidi lakini tuliafikiana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba haya ya sasa hivi ambayo yanashughulikia kanuni ni ya msingi zaidi na hayo mengine yatakuja kwenye Bunge lijalo. Kwa hiyo, mimi naunga mkono kabisa marekebisho haya kwa sababu kama sheria haimpi nafasi Waziri ya kutunga kanuni basi hata utekelezaji wake unakuwa ni wa matatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naunga mkono kabisa marekebisho haya.

Sehemu nyingine ninayopenda kuchangia ni sehemu ya 9 inayohusu Sheria ya Uchaguzi wa Madiwani. Nadhani suala hili limekuwa vizuri kwamba limewekewa utaratibu ambao hauleti migogoro baadaye kwamba yale maslahi aliyonayo mgombea basi mapema kabisa kabla hajateuliwa yaweze kufahamika ili kuondoa matatizo ya kuweza kukosa mgombea na pengine mgombea huyo hakuweza kujua tu nini afanye. Kwa hiyo, naunga mkono kabisa hilo.

Sehemu nyingine ni sehemu ile ya 11 inayohusu Mafao ya Viongozi wa Taifa. Mimi nakubaliana kabisa kwamba ni vizuri yale yanayoingia katika sheria yenyewe yawe ni yale makubwa tu ya pensheni, kiinua mgongo na ufungaji wa shughuli, lakini yale mengine madogo madogo yashughulikiwe kwa utaratibu mwingine kwa sababu ya mabadiliko katika hali ya maisha. Kwa hiyo, mimi naunga mkono kabisa hili.

Lingine ambalo nilipenda kuliongeza hapa labda huenda linatekelezwa kwamba ni vizuri viongozi hawa wastaa fu wasihusike husike sana na *voucher* za Serikali. Kule kusaini saini kule kama kunafanyika hivi wajitahidi kwa njia yoyote wajaribu kupunguza hiyo ya kuwahuishisha na masuala ya ukaguzi. Nadhani hilo lingetafutiwa njia ya namna ambayo wangefanya maisha yao bila kujihusisha na taratibu za uendeshaji wa siku hadi siku wa Serikali. Utafutwe utaratibu tu kwamba ana fungu lake analiendeleza kama lina matatizo basi ni mawasiliano na kiongozi huyo anayesimamia ambaye nadhani ni Waziri wa Utumishi na vyombo vingine, hili litawasaidia sana kuishi maisha ya kawaida. Kwa hiyo, naunga mkono sana marekebisho hayo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nimependa kuligusia hapa ni Tume ya Huduma za Bunge. Nakubaliana sana na marekebisho kwamba Tume ya Bunge iwe na madaraka kuhusu maslahi ya Wabunge maana ndiyo inayojua mazingira ya kazi za Wabunge kwa hiyo, ina nafasi ya kuweza kuelewa ni nini Wabunge watahitaji ili watekeleze kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda kutoa tahadhari kwamba tujitahidi kwa kweli kutohusisha makundi mbalimbali katika mfumo mmoja wakati aina za ajira zao ni tofauti. Kwa mfano uteuzi wa Mkuu wa Wilaya hauna muda, anaweza kukaa mpaka miaka 10 au 15 lakini ana utumishi mwingine unaunganishwa hapo, sasa ukimweka pamoja na mtu mwingine ambaye utumishi wake ni wa muda mfupi wa miaka mitano unaweza kumkoshesha huyu maslahi ambayo yangemsaidia kuishi vizuri huyu wa kipindi hiki kifupi, kwa hiyo, ni vizuri kuyatenganisha hayo. Hawa wa vipindi virefu sheria za pensheni ndizo zinawahusu. Lakini wa vipindi vifupi wasiunganishwe na wale wa vipindi virefu kwa sababu kwanza ukiwahuishisha unaweza kuwa na gharama kubwa sana kwa wale amba wana vipindi virefu vya kazi lakini kwa wale amba wana *contract* ya miaka mitano (*political contract*) na wananchi basi maslahi yao yazungumziwe kipekee na yasihuise wengine kwa sababu hata mazingira yao ya kazi ni tofauti. Kwa hiyo, dosari hizi ndogo nazo zingeweza kuondolewa.

Mheshimiwa Spika, nina mchango kuhusu sehemu ya 13 inayohusu Tume ya Kurekebisha Sheria. Nakubaliana sana na mapendeleko ya kuongeza idadi ya Makamishna. Lakini sidhani kama ni idadi tu zaidi ndiyo tatizo. Tatizo ni uongozaji wa vikao. Kikao ambacho kina wajumbe wanaogawanyika kwa mbili kina matatizo ya *quorum* hata kufika mahali Mwenyekiti anashindwa kutoa uamuzi kwa urahisi. Kwa hiyo kwa utaratibu wa kuongoza vikao (bahati nzuri mimi nimeandika vitabu vya namna ya kuongoza mikutano namba ambazo zinakubalika vizuri zaidi za uongozi katika vikao ni tatu, tano, saba, tisa, kumi na moja, kumi na tatu, kumi na tano, kumi na saba, kumi na tisa, ishirini na moja na kadhalika) kwa sababu *chairman* huyo yuko peke yake (namba isiyogawanyika kwa mbili) hata wajumbe wakigawanyika, wakiwa makundi mawili

bado *chairman* atakuwa na nafasi ya kura yake kwa hiyo huwezi kukuta mahali ambapo kura zinalingana.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono Muswada wote huu. Ahsante sana.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, kwanza *Happy Birthday*.

Napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika Muswada ulio mbele yetu, lengo na makusudi ya kusimama ni kutaka kuunga mkono hoja. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe kwanza salaam za rambi rambi kwa familia ya Marehemu aliyekuwa Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga, kwa wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa kupotelewa na Mbunge wao mpendwa ambaye wamempoteza katika siku za hivi karibuni tunapoelekeea kumalizia kipindi hiki cha Bunge hili.

Baada ya rambi rambi hizo namwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin*.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pongezi za dhati kwa uendeshaji mzuri na makini wa kidemokrasia kwa Mheshimiwa Rais wetu na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa jinsi alivyokiongoza chama chatu tarehe 04 Mei, 2005 kuweza kumpata mgombea wa kiti cha Urais atakayechukua nafasi yake. Nami nawatakia kila la kheri Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Mheshimiwa Aman Abeid Karume, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwamba wakishikilia bendera yetu Mwenyezi Mungu awasadie katika kushinda kwa kishindo kuweza kuongoza madaraka ya nchi hii kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo naomba niseme machache kama ifuatavyo, kwamba katika kipindi hiki ambapo Serikali yetu inaelekeza nguvu zake pamoja katika mwelekeo wa ari mpya, kasi mpya, nguvu mpya na kuhakikisha kwamba inaweka mbele mkakati wa kuondoa umaskini nchini, wa kuinua kipato cha mwananchi, ni wakati muafaka ambapo imeleta marekebisho mazuri kabisa ya kubadilisha hizi sheria mbalimbali ambazo zimewasilishwa na Mwanasheria Mkuu ambapo mojawapo ni ile inayozingatia haki za mwenye nyumba na Shirika la Nyumba linapokuwa na nyumba zake kuweza kuzipangisha kwa lengo la kupata faida.

Mheshimiwa Spika, watu wengi wangependa sana kuishi katika nyumba za Shirika la Nyumba si kwa sababu wanazipenda zile nyumba lakini ni kwa sababu walipata nafasi ya kuweza kuishi katika nyumba zile bila kulipa na bila kubughudhiwa, sasa kwa kuipitisha sheria hii tutawezesha Shirika la Nyumba kwenda kufanya kazi yake ipasavyo vile vile kuweka eneo mojawapo la uwekezaji na kuweza kuwawezesha wananchi kuinua hali yao ya kipato. Kwa hiyo basi Shirika la Nyumba litakuwa ni sehemu ya kufanya biashara na vile vile litakuwa ni sehemu ya kuinua uchumi na itakuwa ni sehemu ambayo sasa wote wanaopenda kuishi Shirika la Nyumba ama

kwenye nyumba yake ama nyumba ya mtu mwingine atawez ka kuwa na haki kama ambavyo mwenye nyumba naye atawez ka kuwa na haki. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kuhakikisha kwamba mwenye nyumba naye sasa anakuwa na haki ya kudai pango lake halali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo wameshazungumza wenzangu, sitaki kurudia, nayaunga mkono lakini naomba tu kuchangia machache kwamba pamoja na kwamba sasa mwenye nyumba atakuwa na haki ya kudai haki yake bila kutakiwa kufika mahakamani ambapo mpangaji na yule mwenye nyumba wataweza sasa kupatana katika mkataba, kuwekeana muda wa kulipa bila kubughudhiana. Bado atakayetaka kwenda mahakamani kwa sababu ni haki yake ya kisheria anaweza akaenda.

Mheshimiwa Spika, bado nilikuwa nafikiria machache yangeweza yakafanyika kwamba wapo wapangaji amba ni wakorofii inapofika wakati wa kutaka kutoka kwenye nyumba hata ukitangaza kwenye vyombo hata ukibandika tangazo bado atakuja kusababisha ukorofii. Bado mimi ningeshauri kwamba wale viongozi wetu wa Serikali za Mitaa wanaokuwa katika maeneo wangeshuhudia ile mikataba ili mikataba ile ikaweza kupata walau nguvu za uongozi uliopo pale hata inapotokea mwenye nyumba anataka kwenda kufungia vyombo vya mpangaji yule ama kubandika tangazo la kuviuza basi kuwe na kiongozi wa Serikali anayeshuhudia ili kuondoa kuzushiwa kwa mwenye nyumba kwamba pengine alikuta vyombo vya milioni 10 lakini yeze kaviuza kwa milioni moja ama kwa laki tano ambavyo ilikuwa ndiyo deni lake, jambo hili lingeweza likawekwa ili kuweza kuweka maeneo yote mawili kupata haki, yaani mpangaji na mwenye nyumba.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ninaloliomba ni kuwaomba wapangaji kutunza nyumba za weny nyumba, wapangaji wamekuwa na tabia moja ya kusikitisha sana labda hata na wengine tunaweza hata tumo ndani ya nyumba hii. Mtu anaingia kwenye nyumba nzuri, anadai kuwekewa kitasa safi, choo safi, mazingira masafi lakini siku anapoondoka nyumba ile inakuwa haitazamiki, anang'oa mpaka na vitasa, anabomoa vyoo, anabomoa milango anafanya vitu vya kutisha kabisa.

Mheshimiwa Spika, naomba na hili liingie katika kuangalia haki ya mwenye nyumba. Nyumba yake anavyoitao safi hata siku yule mwenye kuipangisha anapoondoka licha ya kodi anayolipa sawasawa kwa jinsi anavyotakiwa na sheria lakini lazima aiache ni safi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kuliomba ni kwamba naiomba Serikali sheria hii inapita wakati ambapo hatujajiandaa vizuri kuwahudumia watumishi wetu kule vijijini na katika maeneo mengine ya miji, watumishi wetu wengi watakuwa wanakwenda kuishi katika nyuma za watu binafsi hasa walimu na wataalam wanaoishi vijijini. Sasa naomba basi katika ule msukumo wa MMES na MMEM naomba suala zima la kujenga nyumba katika shule za sekondari na shule za msingi lipewe nguvu zaidi kwa sababu kumekuwa na utaratibu Serikali inachelewa sana kuleta malipo ya walimu hasa weny ajira ya kwanza. Mimi ninamwonea huruma huyu mwalimu wangu atakayepata shida,

akatakiwa aondoke kwenye nyumba akafungiwe vyombo vyake wakati hajapata mshahara mwaka mzima.

Kwa hiyo, naomba utaratibu huu sasa uwajali hawa, mara mwalimu anapoajiriwa isichukue miezi mitatu kwa sababu mkataba atakaoingia wa kwanza kwa kijilinda mathalani utakuwa ni wa miezi mitatu lakini baada ya miezi mitatu atatakiwa kuwa amelipa, sasa atalipa kitu gani, mwanzo wanafadhiliwa na wazazi na wananchi katika jamii inayowazunguka lakini baada ya kipindi lazima hawa waweze kulipa.

Mimi naomba mishahara ya walimu na wataalamu wetu wanaoishi maeneo ya vijiji kwa kweli iwe inawahishwa ili wasije wakaadhiriwa na wakakata tamaa ya kutoa huduma katika sehemu za vijiji.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kuliomba ni la mwisho kabisa ni kwamba lingine ni kuangaliwa, wengine wakishaingia kwenye nyumba hasa za *National Housing* wanapenda kufuga ndani ya yale majumba, wanafuga kuku mle ndani, wanafuga ng'ombe, mbuzi mle mle ndani achana na kujenga uzio nje, ndani ya vyumba mle wanafanya hivyo mambo haya yaangaliwe, waweze kuweka mazingira safi katika zile nyumba na kuendelea kuzitunza zile nyumba.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho kabisa hilo la ufügaji mijini na lenyewe kuangaliwa upya, sasa imageuka kuwa kero harufu mbaya kwa majirani, mifugo kuharibu hata bustani za wenzao sasa hivi watu wanatengeneza tubustani tuzuri iangaliwe na yenyele ili kuweza kuweka mazingira mazuri.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa na la kumalizia ni marekebisho katika Bima ya Afya. Naishukuru Serikali kwa kuangalia na kuweka kile kifungu cha kuwashudumia walimu hasa miwani na huduma zingine muhimu ambazo zilikuwa zimeachwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii na nikuhakikishie kwamba sitatumia dakika zote kumi na tano.

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Kwanza nianze kama wenzangu walivyosema na kwa kifupi sana kutoa rambi rambi zangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Lushoto kwa kifo cha Ndugu yetu Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga.

Pili, nikipongeze Chama Cha Mapinduzi kama kawaida yetu kwa maamuzi mazuri ya kidemokrasia ambayo kwa kweli yameonekana kama mfano katika uteuzi wa Ndugu Jakaya Mrisho Kikwete, pamoja na Rais wa sasa hivi wa Zanzibar ambaye

amerejeshewa nafasi yake agombee tena na pia vile vile Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, ambaye amepewa nafasi ya kugombea kama mgombea mwenza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi nitajielekeza katika eneo la Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 kwa kifupi nina mambo mawili.

Kwanza naomba Serikali hasa kupitia kwa Mwanasheria Mkuu atoe maelekezo au atoe maelezo kuhusu utata uliojitokeza katika maeneo ambayo mabaraza ya ardhi yalichelewa kuanza au yalianza kulikuwepo na maagizo ya Serikali kwamba Sheria ile ya Ardhi itanza kutumika kuanzia Oktoba, 2003 na shughuli za mahakama kusikiliza kesi za ardhi zisitishwe lakini kumekuwepo na utaratibu wa kuendelea mahakama kusikiliza kesi na kesi nyingine kwa kweli zimeamuliwa bila kuangalia utashi. Aidha, mahakimu hawa walijua kwamba sheria ile haitatumika kwa hiyo, uamuzi uliofanyika pengine ni wa uonevu sana katika maeneo mengine sasa je wananchi wale ambao hukumu zilipitishwa wakati sheria haifanyi kazi yaani kuanzia ile Oktoba, 2003 Serikali inatoa kauli gani? Je, hizi kesi zote siyo batili? Tunaomba hii tupate mwelekezo ili wananchi ambao wamesingiziwa kesi zao kwa kipindi kile na wanaona kwamba hawakutendewa haki basi kesi zile zibatilishwe.

Mheshimiwa Spika, lingine ni dogo pia linaelekea katika sheria hiyo hiyo, katika suala la mpangaji na mpangishwaji katika maeneo yaliyo na uhaba wa ardhi kwa mfano Lushoto, kuna maeneo ambayo kuna watu wenye hati na hii nitakuwa muwazi labda Waziri wa Ardhi atanisaidia. Kuna eneo ambalo liko Ubiri, kuna Taasisi ambayo iliomba ardhi kwa madhumuni ya kujenga huduma za jamii katika eneo hilo kwa bahati mbaya Taasisi ile ikachukua hati katika eneo la shamba ambalo lilikuwa linatumia na wananchi na Taasisi ile haikutekeleza ahadi yake. Taasisi hiyo imechukua ardhi ile na inafika hatua ya kuwapangisha wananchi wale wale ambao walitoa ardhi yao kwa ajili ya kupata huduma katika hali ya namna ni chombo gani kitashughulikia mgogoro huu kwa sababu kwa sasa hivi naogopa wananchi wanapangishwa katika maeneo haya ya ardhi inaweza ikavunjika amani kwa mwananchi atakapofuatwa kwamba lipia ardhi uliyokuwa unatumia na sasa hivi unapangishwa hatakubali na huyu atapewa haki ya kumtoa yule katika eneo lile.

Mheshimiwa Spika, hii inaweza kuleta mgogoro mkubwa na naomba Serikali itoe maelekezo wananchi na haki ya kurejeshewa ardhi yao wamuachie yule eneo analolitumia kwa sasa au haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kumalizia hapo kwa kuiomba Serikali na kuunga mkono hoja na kupenda kusema kwamba kwa kweli Muswada huu umekuja kwa wakati muafaka. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia, nianze kwa kukupa wewe *Happy Birthday and how old are you now?* Utanijibu baadaye. (*Kicheko*)

**SPIKA:** *Thank you.*

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Spika, naomba niungane na wenzangu kwa kutoa rambirambi kwa mwenzetu ambaye ametutoka Hayati Abu Kiwanga, roho yake ikae mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, niendelee kwa kuipongeza Serikali kama wenzangu walivyofanya kwa kuleta marekebisho haya, marekebisho yamekuja wakati muafaka na mimi ningependa nizungumzie vipengele viwili tu.

Mheshimiwa Spika, kipengele cha kwanza ni kuhusu Shirika la Nyumba, kwa ujumla marekabisho haya yatasaidia sana katika mahusiano ambayo yalikuwa kwa kweli ni mabaya baina ya wapangaji na wale ambao wanapangishwa nadhani sasa itatusaidia kwa kupunguza nguvu kubwa ambayo walikuwa nayo wapangaji.

Mheshimiwa Spika, ninayo machache ambayo ningependa hasa kuwa-*direct* kwenye Shirika la Nyumba la Taifa hasa katika upandishaji wa kodi, sheria imetoa vigezo, nitazungumzia kigezo kimoja tu nacho ni kigezo cha hali ya nyumba.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kama cha miaka miwili au mitatu iliyopita Shirika limekuwa likipandisha kodi nyumba hizi kwa kasi kubwa sana, si vibaya kufanya hivyo lakini baya kubwa ambalo limejitokeza ni kwamba Shirika lilikuwa likipandisha kuangalia zaidi, kigezo cha ukubwa lakini ilisahau kigezo cha ubora wa nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, hali ya nyumba za *National Housing* ni mbaya sana na kwa zile chache ambazo zinaonekana zinatiwa rangi mbele ya nyumba ambazo ni kama mitaa mikubwa ya Dar es Salaam ili watu wakipita waone nyumba za *National Housing* hakuna matengenezo ya ndani hata siku moja.

Mheshimiwa Spika, ukienda katika maeneo ya Keko, Ilala, Kota za Ilala, Kota za Ubungo ni sehemu ambapo huamini kama wanaishi watu, ukitoka unakutana na mabwana ya maji machafu, ni uchafu mtupu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naamini hivi vigezo vitatumika navyo ili kuwapandishia, ikumbukwe tu wale wananchi wanaokaa katika nyumba hizi za *National Housing* wanajisikia unyonge sana kulipa hizi kodi kutokana na hali mbaya ya nyumba zenyewe, wanatumia pesa nyingi kujitengenezea, kutengeneza mabomba na hata kutengeneza milango.

Mheshimiwa Spika, katika nyumba hizi za *National Housing* kuna watu wamekaa toka zijengwe wamo mle ndani, hamna *repair* yoyote inayotengenezwa ndani kuna wengine wako katika nyuma hizi tangu zitaifishwe hakuna *repair* yoyote kwa hiyo *National Housing* huu ni wakati wa kutumia Sheria hii kupandisha kodi lakini kuzitengeneza nyumba hizi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni kuhusu kuipa meno, sheria hii imeipa meno Shirika la Nyumba kuijiendesha kibashara, basi

nimeshasema sana katika Bunge hili kuhusu nyumba hizi za *National Housing* ziuzwe kwa wale wanaoishi mle ndani ili Shirika lipate uwezo wa kuweza kujenga nyumba nyingi zaidi. Haitoshi zile nyumba chache zinazojengwa ingeweza ikajenga nyumba nyingi zaidi kama isingeng'ang'ania vile vighorofa vinavyokaa watu pale katikati ya mji wale hawatohama hata siku moja kwa hiyo ni vema kama zikiuzwa kwa wananchi wale ambaao wako mle ili waweze kujenga nyagine.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaonyesha mfano, imeuza nyumba kwa wale ambaao wanakaa, wengine wamekaa miaka miwili tu wameuziwa zile nyumba lakini hawa wananchi wamekaa zaidi ya miaka 20, 30 na hata 40 lakini wanalipa kodi tu, wanalipa kodi hakuna *repair* ya nyumba. Kwa hiyo, kwa Muswada huu nadhani wananchi watakuwa wamefurahi sana kwa kuona kwamba nyumba hizi nazo zitauzwa kama vile nyumba za Serikali zilivyouzwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu umetuambia muda hakuna ningependa nizungumzie Tume, Tume ya Huduma za Bunge. Ni vema sana ilivyofanywa kuwapa uwezo kwa sababu ni Tume ya Bunge peke yake ambayo inaweza kujua matatizo ya Wabunge na kujua mafao yao yaweje.

Mheshimiwa Spika, lakini moja ningependa kulizungumza na ni ushauri tu, Tume ya Huduma za Bunge isiwe kwa kipindi cha miaka mitano yote, nashauri Tume ya Huduma za Bunge iwe kwa kipindi cha miaka miwili na nusu halafu tunachagua nyingine kwa miaka miwili na nusu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninasema hivyo kwa sababu hata ile Tume inapokuwa haiku-deliver matarajio yetu bado inabidi tukae nayo miaka mitano. Tunaone hata katika mashirika, *Board* zinakaa miaka mitatu basi sisi tunaweza tukakaa hata miaka miwili na nusu ili tuweze kupata wengine kama wale ambaao wapo wanaweza wakarudia kama wanafanya kazi nzuri lakini ni vema kama hili jukumu kama vile tunavyofanya Kamati za Bunge zinavyokuwa kipindi cha miaka miwili na nusu na miaka miwili na nusu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana hapo ndiyo tunafikia mwisho wa orodha ya wale walioomba kuchangia kwa mdomo, sasa ..

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Pawa!

**SPIKA:** Aah! Pawa sijamuita, ooh! Samahani Rais wa awamu ya nne aliukosa sasa nime... Mheshimiwa Semindu Pawa. (*Kicheko*)

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana nilijua tu *it is a joke of the day*.

Mheshimiwa Spika, nasimama mbele yako kutoa maoni machache tu, lakini kabla sijafanya hivyo ningependa nitoe salaam za rambi rambi kwa kifo cha Mheshimiwa Abu

Kiwanga, kwa familia yake na pamoja na wapiga kura wake, mimi niliwakilisha Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli wananchi wa kule wameupongeza sana uongozi wako kwa utaratibu ambao umeufanya, Katibu wa Bunge na Waheshimiwa Wabunge kwa michango ambayo tumeitoa kule tumewakilisha barabara na wananchi walifurahi sana kwa uwakilishi ule.

Mheshimiwa Spika, niliwaambia kwamba Mheshimiwa Abu Kiwanga, mlimpenda lakini Mungu alimpenda zaidi na amemchukua alivyompenda mwenyewe wakati huo. Mungu amweke mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, nasema, haya ni matokeo hutoweka, si majoribu maana majoribu hujaribika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nasema zote zinazozungumzwa kusema kweli hapa ni barabara, yapo mapungufu yalijitokeza ili kuongeza vipengele kadhaa ili kuwa na uendeshaji mzuri wa Miswada na sheria zilizokuwepo hapo awali.

Mimi najikita katika Sheria ya Ardhi. Katika mwaka 1999 tulipitisha Sheria ya Ardhi Vijijini na Mijini. Sasa nataka kuuliza, je, kwa nini Mijini kuna baadhi ya mashamba makubwa na maeneo makubwa kuliko maeneo ambayo sheria inavyosema katika Miji?

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu mipaka ya Vijiji, migogoro hii inaendeshwa mpaka lini? Tatu, migogoro ya wafugaji na wakulima nani anayesuluhisha? Nne, mashamba yasiyoendelezwa katika maeneo ya Vijiji ambayo wananchi wanataka kuyalima, kwa nini Madiwani wa maeneo haya wasipewe madaraka kutoa mapendekezo, sio ku-revoke, kazi ya ku-revoke ni kazi ya Rais. Sasa yatolewe mapendekezo kwa baadhi ya mashamba hayo ili kusudi wananchi wayachukue na kuyalima baada ya kubaki mapori wakati wananchi wanakwenda kulima maeneo ya mbali. Vipo vyombo vingi lakini kwa sababu wananchi hawajui mahali gani waende, wamekwenda kwenye Tume ya Haki za Binadamu, kwa Waziri wa Ardhi, kwa Mkuu wa Mkoa, kwa Mkuu wa Wilaya na kwa Mbunge mpaka wengine wanaomba nafasi ya kwenda kwa Rais.

Kwa hiyo, hii italeta vurugu kutokana na mkanganyiko wa mahusiano ya utekelezaji wa nani atoe haki katika maeneo haya. Sasa Baraza hili nadhani na vyombo vya Sheria, kwa mujibu wa sheria hii basi watapewa ufuutiliaji wa mambo haya.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu Bima ya Afya. Bima ya Afya ni chombo cha huduma, sio chombo cha uzalishaji fedha. Kwa hiyo, ndiyo maana haikuelekezwa kwa mujibu wa *financial regulations*, imeundwa kwa ajili ya masuala ya huduma kwa ajili ya wafanyakazi wetu na tulipongeza sana na tunampongeza Waziri wa Afya wa awali na wa hivi sasa na wananchi wanafurahia sana maendeleo yake. Matatizo yapo ambayo ni mapungufu kadhaa ambayo yamejitokeza. Mapungufu yenye ni kama yafuatayo:-

(a) Yapo manung'uniko mengi sana wanayatoa hususan walimu ambao ni wadau wakubwa katika mfuko huu ya kwamba kuwekewa *sealing* katika kiasi cha madawa ya kununua wakati wanapoumwa.

(b) Kuna matatizo mengine ambayo yamejitokeza kuhusu masuala ya watu wawili ambao ni wanachama, mke na mume ambao wote huchangia mfuko huu. Sasa nani tegemezi kwa mwenzake, lazima kuwepo na taratibu na *regulation* ilitolewa na Wizara ya Afya ili kuona kwamba achangie mmoja kati ya hao.

(c) Vile vile *sealing* ya watoto kweli ukiwa na watoto sita au saba ni watoto wako. Kwa hiyo, huwezi kuchagua watoto wangapi ndio watakuwa ni watoto wako ili wawze kutibiwa na wengine wabaki. Sijui kama hili limerekebishwa katika sheria hii. Wale ni wanachama na wadau, idadi ya watoto na ukomo wa fedha ya tiba si vizuri katika mfuko wa huduma kama huu kwa sababu haifuati *financial regulation* ni mfuko wa huduma. Wanachama mke na mume nimesema kwamba wanakatwa mishahara, basi hilo niliweke katika hali hiyo kwa sababu ya haki ya tegemezi kwa mke na mume.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, napenda kusema kwamba Tanzania tunajiamini na pongezi kwa kujiamini, kujitegemea, kujiedeleza, baadaye tukifanikiwa tunajivunia. Vile vile mambo mengine mabovu tunayapuuza bila ya kuyadharau na kebehi, tunaviachia vitu na kuvitupilia mbali bila ya kukashfu na dharau na masimango. Vile vile tunatupilia mbali vishawishi, majoribu na vitu vya matokeo bila ya bugudha, tunakwenda mbali na tunasonga mbele kwa hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, Miswada iliyoko mbele yetu ni sahihi kabisa kwa sababu si mipyä, inafanya marekebisho ya Miswada iliyokuwepo katika nchi hii. Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ila yale mapungufu yazingatiwe na Waziri anayehusika. Ahsante sana. (*Makofî*)

**SPIKA:** Tunampa muda kidogo mtoa hoja ajiandae kwa kutoa majibu ya hoja yake. Wakati anajiandaa Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe kwamba kipindi cha mchana kinaanza saa kumi kama jana. Rais na Makamu wa Rais pamoja na wageni wao niliowatambulisha jana watakuwa wameshafika kabla ya saa kumi ili kusudi tuweze kuanza saa kumi kamili kama tulivyopanga.

Waheshimiwa Wabunge, tutakuwa katika mkao ambao si wa Bunge, lakini mkao wa semina. Kwa hiyo, wageni wetu wataingia kwa utaratibu usiokuwa wa Kibunge. Wataingia kutoka *Speaker's Lounge*, halafu tutakaa, meza hizi zitakuwa zimeshabadilishwa, halafu watoa mada, Rais, Makamu wa Rais, Spika na wageni wa Rais tutakaa nao huku juu. Patakuwa na *podium* hapa ya kutolea ile *lecture* na wakati wa kuzindua kitabu kuna wageni fulani fulani, sio wageni lakini ni Watanzania ambao wanaongoza maeneo, ambao wanaitwa *public opinion leaders* nafikiri, wanaongoza maeneo fulani fulani ambao tutawewekea viti hapa, wapo kama kumi na nane hivi, ili kusudi baada ya kuzindua ile ripoti Mheshimiwa Rais atawakabidhi mmoja mmoja ili wakavitumie kwenye maeneo yao kueneza ujumbe ulioko kwenye ripoti hiyo. Hivyo ndivyo tulivyopanga.

Kwa hiyo, naomba tuje tumejiandaa, hivyo tuwahi kikao kwa sababu viongozi wetu wa Kitaifa watakuwepo na ndio maana hata ukumbi wa Bunge umebadilika sura yake kwa sababu ya ugeni huo unaokuja. (*Makofi/Kicheko*)

**WABUNGE FULANI:** Na kwa ajili ya *birthday*. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Kwani ni *birthday* ya nani leo?

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu *part x, Practitioners and Dentists Ordinance*, nakubaliana na hoja kwamba kwa daktari aliyesajiliwa Tanzania Zanzibar kusiwe na ulazima wa yeze kujisajili Tanzania Bara endapo ataamua kufanya kazi Bara.

Mheshimiwa Spika, vile vile napendekeza kuwekwe kipengele katika Sheria kinachotamka wazi kwamba Daktari aliyesajiliwa Bara asilazimike kujisajili upya Zanzibar kama atataka kufanya kazi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, usajili wa madaktari ni tofauti na ule wa sekta ya wafanyabiashara wa mifumo ya kodi. Usajili wa madaktari unalenga kumlinda mwananchi licha ya kupata na kutunza orodha ya madaktari waliopo nchini, tunataka madaktari walio Bara wenye kisomo kisicho na shaka, wenye uzoefu wanaozingatia maadili. Hii ina maana kwamba ni muhimu kuwa na chombo cha *ku-screen* madaktari waliosomea udaktari nchi za nje. Chombo hicho ama kiwe kimoja kwa Bara na Zanzibar au vigezo viwe vya namna moja. Vinginevyo, masharti yakiwa nafuu upande mmoja basi madaktari watajisajili upande mmoja lakini wakaenda kufanya kazi upande mwingine wa Jamhuri.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo ya mabadiliko yaliyoletwa na Serikali ukurasa wa 4, kifungu cha (3), ningombwa kupewa ufanuzi wa kiutekelezaji unaoweza kuendana na mapendekezo katika kifungu hicho cha (3) *in case of International Non Governmental Organization, the application for registration shall be submitted by one or more persons, being the founder members and two of whom shall be residents of Tanzania.*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hapo juu Sheria imeruhusu kwamba *registration* inaweza kufanyika na *founder member* mmoja na hapo hapo Sheria inadai katika *registration* lazima *two resident* wa Tanzania wawemo katika *registration*, nafikiri hapo Sheria inakinzana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mara zote mabadiliko ya Sheria husaidia sana kuondoa migongano ya kiutekelezaji ya Sheria husika, katika Kamati nilipendekeza katika kufanya mabadiliko ya kifungu kinachohusu Bodi ya *NGO*, basi mionganoni mwa

kazi za Bodi iwe ni pamoja na kuangalia uwiano wa maeneo ya kufanya kazi ya *NGOs* hizo husika ili kupunguza mlundikano wa *NGOs* hizo katika eneo moja.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kutoa salaam za rambirambi kwa wananchi wote wa Kilombero kwa kufiwa na Mbunge wao Mheshimiwa Abu Kiwanga.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuteuliwa kuwa mgombea Urais kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hoja hii, pamoja na mapendekezo yanayoletwa hapa katika mafungu ya 34, 35 na 36 naomba pia nibainishe maeneo mengine yanayohusiana na Bima ya Afya kwa wafanyakazi, wafanyakazi wanalamikia huduma zitolewazo na Mfuko huu wa Bima ya Afya. Wanaomba utaratibu wa sasa urekebishwe ambapo ni baadhi tu ya magonjwa yanatibiwa. Mara nyingine hata upasuaji hauhusishwi katika matibabu lakini wafanyakazi wanakatwa mishahara yao kila mwezi ingawa hawaumwi kila mwezi. Serikali ifikirie kubadilisha/kurekebisha eneo hili la Bima ya Afya ili likidhi mahitaji ya tiba kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, pia wafanyakazi wanapostaifu au kufariki pamoja na kwamba wamechangia kwa muda mrefu basi huondolewa au familia zao huondolewa mara moja katika utaratibu wa matibabu. Nashauri hili liangaliwe angalau kwa kiwango ambacho mhusika amechangia na kama rekodi inaonyesha ni gharama gani ameshatumia mchango wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa mtoa hoja kama upo tayari tafadhali hitimisha hoja yako.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii ili sasa niweze kuhitimisha hoja hii. Lakini kama ilivyo kawaida nianze kwa kuwatambua na kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii nikianza na wale waliochangia kwa kuzungumza humu Bungeni. Naanza na Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua Muswada huu, Mheshimiwa Athumanji Janguo, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Sophia Simba na mwisho kwa kutajwa tu ni Mheshimiwa Semindu Pawa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ninao Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa na Mheshimiwa Damas Nakei. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao wamesikiliza hoja, wameielewa na ndio maana hawakuomba nafasi ya kuchangia aidha kwa maandishi au kuchangia kwa kusema. Nawashukuruni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naamini hoja inajieleza yenyewe na haihitaji maneno mengi lakini yapo machache tu ambayo ni vizuri nikayasemea. Nianze tu moja kwa moja na hili la hizi nyumba zinazokodishwa au maeneo yanayokodishwa.

Kwa upande wa nyumba, rai ya Mheshimiwa Eliachim Simpasa na nilisikia pia kwa Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, tumesikia ushauri wao kwamba Serikali isitofautishe aina ya matumizi ya nyumba kwamba kuna hii ya makazi na hii ya biashara. Kama mtu hajatekeleza yale aliyoyakubali maana hakulazimishwa kufika pale, alifika kwa hiari yake na amekubali kwamba nitatekeleza makubaliano. Moja kubwa, ni pango la nyumba, sasa hawezi akasema kwenye makazi anaweza tu akasema ahsante baba nipo tu lakini halipi pango. Lakini nasema kwa sababu hiyo sasa inapendekezwa masharti tumeweka sasa sababu hiyo haya yatahusu nyumba zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikiwa katika eneo hili nataka pia nimhakikishie Mheshimiwa Eliachim Simpasa, kwanza nimshukuru sana kwenye Kamati ametusaidia sana maana sikujuu kwamba yupo katika sehemu mbalimbali hasa katika eneo hili ametusaidia sana na nimhakikishie tu kwamba ndio maana tumekiangalia upya kifungu cha 101 cha Sheria hiyo ya Ardhi. Pia sasa hivi tutakapofika kwenye Kamati ya Bunge Zima nataka niseme tu kwamba kifungu cha 102(1) ambacho tumeonyesha katika orodha ya marekebisho napendekeza tukifanyie marekebisho kidogo kwa kuanza katika kifungu kidogo cha kwanza kwa kusema *subject to subsection three*: “*A lessor may, unaendelea sasa yaani tutakapofika kwenye kifungu kidogo cha tatu hapo tutasema the exercise of the right levy distress may only be exercised using a Court broker or a broker of a Tribunal.* Sasa hii ndio tunasema mahali ambapo hapatakuwa na uvunjifu wa amani kama tunavyo-set out hiyo hii haki ya mwenye nyumba ya ku-levy distress yaani kukamata zile mali za mpangaji ambaye anakuwa mkaidi tu kutokulipa na uzoefu umeonyesha, pale ambapo mpangaji mkaidi anaona kwamba mmh, siku ya siku imefika wanakusanya mali, wanataka kuuza atalipa, tena wanakimbia haraka sana kama suala ni kwenda kulipa kodi ya pango. Kwa hiyo, mimi nadhani hiyo tumezingatia na nataka nimhakikishie sana rafiki yangu Mheshimiwa Eliachim Simpasa kwamba hilo liko sawa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ruth Msafiri, anasema nyumba hazikaliki, inapangishwa tu hata kama ukiitengeneza wanakuja kuchafua. Serikali imepitisha Sheria ya Ardhi inaisimamia sheria hiyo na wenyewe nyumba na wapangaji wenyewe lazima wazingatie masharti ya Sheria hii kwa sababu ni sheria ya nchi. Sasa Sheria ya Ardhi inatoa wajibu kwa mwenye nyumba kuitengeneza nyumba hiyo ili iweze kukalika na binadamu isiwe katika mazingira kama ya kukaa wanyama. Vile vile anayepangishwa ana wajibu wa kuhakikisha kwamba nyumba hiyo aliyokubali kupanga iko katika hali ya matumizi yale yale aliyopewa na mwenye nyumba huwezi kuingia na kuanza kubomoa nyumba yangu. Sasa hii utakuwa unakiuka maelewano ya matumizi ya nyumba hiyo. Hiyo ndio sheria.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kuhusiana na *NGOs* za kutoka nje, iwe ni sharti kwa Watanzania kwamba na wenyewe wawemo. Tunaipokea lakini ina tatizo. Kwanza, nizishukuru sana hizi *NGOs* za ndani na nje ambazo zinaisaidia Serikali katika kutoa huduma mbalimbali hasa za kijamii hapa nchini.

Naamini kwa vile wanakuja kwa hiari, Sheria hii inachofanya ni kuwaratibu tujue huko walipo na wanafanya nini na kwa sababu mtazamo sasa hivi wa nchi nyingi duniani ambazo tunashirikiana na Serikali katika kuinua hali ya maisha ya watu wetu zinatoa sehemu kubwa ya rasilimali kupitia vyombo hivi. Ni vizuri tukavitambua, lakini basi kama Serikali ni vizuri tukajua wanafanya nini hapa na pale inapowezekana Halmashauri zetu katika kupanga mipango yao wakaingiza katika mipango yao kwa kushirikiana na hawa, ndio maana tunasema twende nao kwa pamoja kwa maridhiano.

Mheshimiwa Spika, tusilazimishe mtu kwa kupitia sheria kwamba lazima uwe hivi kama unataka kuja hapa na hawa wanatoa huduma na tuseme moja kupitia marekebisho haya tunasema *NGOs* hizi ili waweze kuwa na sifa hizo, mojawapo ni kwamba iwe *non-profit sharing*, hizi hela wanazoletewa isiwe wanakaa katika mkao wa kugawana na kula, hapana. Ukiwa na sura hiyo tunasema hapana, wewe sio *NGO*, zielekeze hizo pesa au rasilimali kwenye maeneo ambayo uliomba kusajiliwa na Katiba yako inasema kwamba utafanya shughuli hizo. Tunawakaribisha waje lakini na wenyewe wajue kwamba kuna taratibu na kanuni za kutekeleza majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, lingine, kupitia eneo hilo la Sheria ya *NGOs*. Tunakubaliana kwamba Chama cha Siasa kinaweza kuanzisha *NGO* yake kwa madhumuni ambayo yanatajwa na sheria ambayo *basically* ni kwa maendeleo ya watu wetu, huwezi kukataza hilo. Tunachosema kupitia marekebisho haya ni kwamba *NGO* hiyo haitatumika kama mbadala wa Chama cha Siasa, ndio Serikali inavyosema. Ukianza mchezo huo tunasema wewe sio *NGO*, nenda ukajisajili kama Chama cha Siasa. Tunawakaribisha wafanye hayo wanayotaka lakini wafanye ndani ya sheria. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jenista Mhagama, alisema kwenye Kamati na amelisema kwenye mchango wake kwa maandishi kuhusiana na *International NGOs*. Muswada ulivyoandikwa ulikuwa kidogo unachanganya, lakini namwomba aangalie sasa hivi katika marekebisho badala ya muasisi mmoja, tunesema waasisi watatu au zaidi na wawili wale sasa wawe wanaishi hapa Tanzania, maana tunataka tufuutilie shughuli zao na uwajibikaji uwe wa wazi.

Mheshimiwa Spika, mambo ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni kuingizwa katika orodha, ahaa, yanazungumzwa, lakini mimi nisingependa, haya yana utaratibu wake, nitakuachia wewe katika wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, hili la Mheshimiwa Henry Shekiffu, mimi nimelisikia hapa na maadamu linagusa masuala ya *circular* iliyotolewa na Serikali na pia maamuzi mengine yaliyotolewa na Mahakama zetu ni vizuri kabla mimi sijalitolea kauli kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni vizuri nikapata taarifa zote na maamuzi yote yalivyokuwa halafu ndio Serikali inaweza kusema. Lakini kwa jitihada ya Serikali sasa

hivi haya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, mimi naamini Serikali imejitahidi sana sasa na yanaanza kufanya kazi tulichelewa kuanza, lakini afadhali kuchelewa kuliko kutokufika kabisa katika jambo hili. Tutajitahidi kadri ya uwezo wetu kuyapatia rasilimali ya kutosha ili yaweze kufanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kusema kweli, nirudie tu kukushukuru wewe na Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano ambao wameipatia Serikali katika Muswada huu na mimi shukrani hizi za uelewa wa Muswada huu nitazifikisha Serikalini hasa katika maeneo muhimu ambayo mmeyatolea maoni na mmeyakubali. Baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea. Katibu.

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### **Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2005** *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments (No. 2)) Bill, 2005)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mambo sio marefu sana, kwa hiyo, nitaomba Katibu asome kifungu kwa kifungu, tutapitisha kifungu kwa kifungu. Karibu Katibu.

Kifungu cha 1  
Kifungu cha 2

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebishi yake)*

Kifungu cha 4

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 5

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 6

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 7

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 8

Kifungu cha 9

Kifungu cha 10

Kifungu cha 11

Kifungu cha 12

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 13

Kifungu cha 14

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 15

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 16

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 17

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nahitimisha hoja yangu nilisema kwamba katika ibara hii tunapendekeza kifungu cha 102(1) tukifanyie marekebisho ili kisomeke kama ifuatavyo.

Napenda sasa iingie kwenye *Hansard*; *Subject to subsection three: "a lessor, halafu yanaendelea kama yalivyo. Halafu kwenye kifungu kidogo cha tatu*

isomeke: “*The exercise of the right levy distress shall only be exercised using a Court broker or a broker of a Tribunal.*” Naomba kuwasilisha.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebishi yake*)

Kifungu cha 18

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebishi yake*)

Kifungu cha 19

Kifungu cha 20

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 21

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebishi yake*)

Kifungu cha 22

Kifungu cha 23

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 24

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebishi yake*)

Kifungu cha 25

Kifungu cha 26

Kifungu cha 27

Kifungu cha 28

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 29

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebishi yake*)

Kifungu cha 30

Kifungu cha 31  
Kifungu cha 32  
Kifungu cha 33

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 34

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebishi yake)*

Kifungu cha 35  
Kifungu cha 36  
Kifungu cha 37  
Kifungu cha 38

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 39

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebishi yake)*

Kifungu cha 40  
Kifungu cha 41

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 42

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebishi yake)*

Kifungu cha 43

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 44

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebishi yake)*

Kifungu cha 45  
Kifungu cha 46  
Kifungu cha 47

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 48

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na  
marekebishi yake)*

Kifungu cha 49  
Kifungu cha 50  
Kifungu cha 51  
Kifungu cha 52  
Kifungu cha 53  
Kifungu cha 54  
Kifungu cha 55  
Kifungu cha 56

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na  
marekebishi yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2005**  
*(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2005)*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2005 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2005*) kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebishi yaliyofanywa. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2005 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2005*) sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria wa Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyokuwa mmetangaziwa na Mheshimiwa Spika, hapa ndiyo mwisho wetu. Kwa hiyo, kwa leo kwa shughuli za Bunge ndio tunazimalizia hapa na kwa hatua hiyo sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 6.05 Mchana Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa  
Tarehe 10 Juni, 2005 saa tatu asubuhi)*